DEPARTMENT OF LINGUISTICS

UNIVERSITY OF ILLINOIS AT URBANA-CHAMPAIGN

# Intermediate Swahili

Supplemental Course Materials



2016-2017

# GENERAL COURSE OBJECTIVES

This course is designed to build on the basic language skills learned at the elementary level. The main objectives of this course include:

- Develop the ability to comprehend extended texts
- Develop ability to write connected paragraphs
- Expand conversational ability
- Increase working vocabulary beyond everyday commonalities
- Build on grammar to enable more effective communication.
- Further understanding of Swahili-speaking cultures in East Africa and beyond

By the end of the course, students should be able to:

1. Demonstrate sufficient comprehension of simple and extended texts
2. Identify main ideas in texts
3. Demonstrate use of a wider range of vocabulary in a variety of situations and consistent with this level
4. Demonstrate improved speaking skills by preparing and presenting oral reports and engaging in conversation on a variety of everyday situations
5. Describe people, places and events
6. Answer in detail and ask questions in highly frequent situations.
7. Show ability to write simply about highly frequent but current events or daily situations
8. Demonstrate an understanding of Swahili culture by using appropriate verbal and non-verbal communication
9. Show a level appropriate control of frequently used morphological and syntactic structures (improved grammar and sentence construction)
10. Show ability to compare their own culture and cultures of the Swahili speaking world.

# Resources

You will need

1. Awde, N. (2000) Swahili-English, English Swahili Practical dictionary
2. Access to memrise https://www.memrise.com/course/955044/furahia-kiswahili/
3. Access to H5P https://h5p.org/user/123223
4. Access to the Swahili Media Space

# FAMILIA

## Msamiati

Jifunze msamiati huu. Fanya zoezi katika memrise:
https://www.memrise.com/course/955044/furahia-kiswahili/

| | | | |
|---|---|---|---|
| binti | *daughter* | mpwa | *nice/nephew* |
| wazazi | *parents* | shangazi | *aunt* |
| bibi/nyanya | *grandmother* | mtoto wa kiume | *male/boy child* |
| babu | *grandfather* | mtoto wa kike | *female/girl child* |
| kitinda mimba | *last born* | kifungua mimba | *first born* |
| mjomba | *uncle* | Mama mkubwa | *father's older sister* |
| mjukuu | *grandchild* | mume | *husband* |
| mke | *wife* | wifi | *sister-in-law* |
| wifi | *sister-in-law* | shemeji | *brother-in-law* |
| mama mkwe | *mother-in-law* | baba mkwe | *father-in-law* |
| mkwe | *daughter/son-in-law* | kitukuu | *great-grandchild* |
| mapacha | *twins* | baba mdogo | *father's younger brother* |
| binamu | *cousin* | ndugu | *sibling* |

## Kusoma

Soma juu ya familia ya Fatma na ujaze mapengo na msamiati huu.

| | | | |
|---|---|---|---|
| dada | wazazi | babu | kaka mdogo |
| binamu | mjomba | shangazi | ndugu |

## Ukoo wa Malaika

Mimi ni Malaika. Nina 1. ---------------------------- watatu: kaka wawili na dada mmoja. Kaka yangu mkubwa anaitwa Hassan na 2.---------------------------- anaitwa Sharifa. Jina la dada yangu ni Tausi. Kaka zangu, dada yangu na mimi tunaishi na 3. ----------------------------wetu katika mji wa Nairobi. Wazazi wangu wanafanya kazi mjini Nairobi. Kaka yangu mkubwa anafanya kazi pia. Mimi na dada yangu tunasoma katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Kaka yangu mdogo anasoma katika shule ya upili ya Hillcrest. Wakati wa likizo, sisi hutembelea bibi na 4. ----------------------------yetu. Bibi na babu wanaishi katika kijiji cha Kajiado. Babu na bibi ni wazee sana kwa hivyo hawatutembelei. Hawawezi kwenda safari ndefu. Bibi yangu ni mkulima. Yeye hukuza mahindi, maharagwe, matunda na mboga. Babu yetu ni mfugaji. Anafuga ng'ombe na mbuzi. 5. ---------------------------- wangu Abdullah anaishi na bibi na babu. Abdullah ni kaka yake mama. 6. ---------------------------- yangu Nafisa ndiye mke wake Abdullah. Shangazi Nafisa na mjomba Abdullah ni walimu. Wanafundisha katika shule ya msingi ya Kajiado. Wao wana watoto watatu. Wao ni 7. ---------------------------- zangu na ninawapenda sana. Wanasoma katika shule ya upili. Ninawapenda babu na bibi pia. Ninafikiri pia wao wananipenda.

### Zoezi

Baada ya kujaza mapengo katika fungu hili, jibu maswali ya ufahamu yafuatayo.

**Maswali**

1. Malaika na familia yake wanaishi wapi?

   ……………………………………………………………………………………………

2. Malaika ana kaka wangapi?

   ……………………………………………………………………………………………

3. Kaka mkubwa wa Malaika anaitwa nani?

   ……………………………………………………………………………………………

4. Tausi ni nani?

…………………………………………………………………………………………

5. Bibi yake Malaika anaishi wapi?

    …………………………………………………………………………………………

6. Babu ya Malaika anafanya kazi gani?

    …………………………………………………………………………………………

7. Mjomba wake Malaika anafanya kazi wapi?

    …………………………………………………………………………………………

8. Malaika na familia yake hutembelea bibi na babu yake lini?

    …………………………………………………………………………………………

9. Kwa nini bibi na babu hawatembelei familia ya Malaika?

    …………………………………………………………………………………………

10. Malaika ana binamu wangapi?

    …………………………………………………………………………………………

## Mazungumzo

**Bi Kidude amepata wajukuu**

*(Mzee Katana na Bi Kidude wamekutana barabarani katika kijiji cha Mtopanga)*

Mzee Katana: Hujambo Bi Kidude! Habari gani?

Bi Kidude: Nzuri sana Bwana Katana. Habari za siku nyingi?

Mzee Katana: Salama tu. Habari za **watoto** na **baba** yao?

Bi Kidude: Wote wazima.

Mzee Katana: Sijakuona siku nyingi sana. Labda tunaweza kwenda mkahawani hapa karibu tunywe chai.

**Bi Kidude:** Asante lakini sitakunywa chai leo. Nina haraka kidogo.

**Mzee Katana:** Unaenda wapi?

**Bi Kidude:** Ninaenda kumwona **binti** yangu Rehema.

**Mzee Katana:** Simfahamu Rehema.

**Bi. Kidude:** Humjui binti yangu yule **kifungua mimba**? Anaishi Nakuru mjini.

**Mzee Katana**: Ooh. Ni yule msichana ambaye aliolewa na Chifu?

**Bi Kidude**: Eeh. **Mume** wake ni Chifu Kariuki.

**Mzee Katana**: Ninamjua. Sijamwona miaka mingi.

**Bi Kidude**: Rehema na mume wake walipata mtoto wiki jana.

**Mzee Katana**: Alipata **mtoto wa kike** au **wa kiume**?

**Bi. Kidude**: Mtoto wa kike. Anaitwa Neema. Ana watoto wengine wawili wa kiume.

**Mzee Katana**: Watoto ni baraka kutoka kwa mungu. Uzee pia ni baraka.

**Bi. Kidude**: Ndiyo: Mimi na mume wangu ni wazee sasa. Tuna **wajukuu** sita.

**Mzee Katana**: Kweli?

**Bi. Kidude**: Eeh. Hamisi na **mke** wake Daniela walipata **mapacha** mwaka uliopita.

**Mzee Katana**: Hamisi ni yule mtoto wako ambaye anaishi Marekani?

**Bi. Kidude**: Ndiyo. Yeye na mke wake walienda Marekani miaka sita iliyopita.

**Mzee Katana**: Sasa watoto wako wote wameondoka nyumbani?

**Bi. Kidude**: Hapana. Rhoda anaishi na sisi bado.

**Mzee Katana**: Rhoda ndiye **kitinda mimba,** sivyo?

**Bi. Kidude**: Ndiyo. Anasoma katika shule ya upili ya Rusinda.

**Mzee Katana**: Aah kumbe! Nilimwona akiwa **mtoto mchanga** sana.

**Bi Kidude**: Ni msichana mkubwa sasa. Ana miaka 16.

**Mzee Katana**: Vizuri.

**Bi Kidude**: Nitaondoka sasa. Salimu mke wako na watoto.

**Mzee Katana**: Nitawasalimu. Kwaheri.

**Bi. Kidude**: Kwaheri ya kuonana.

## Zoezi

**Ni nani kwake?**

*Describe the following familial relationships by completing the phrases.*

Kwa mfano:

(i) Bi. Kidude kwa Rhoda: *Bi. Kidude ni mama ya Rhoda.*

(ii) Neema kwa Rehema: *Neema ni binti ya Rehema.*

1. Rehema kwa Bi. Kidude: ----------------------------------------------------------
2. Rehema kwa Chifu Kariuki: ----------------------------------------------------------
3. Bi. Kidude kwa Rehema: ----------------------------------------------------------
4. Hamisi kwa Rhoda: ----------------------------------------------------------
5. Neema kwa Rehema: ----------------------------------------------------------
6. Hamisi kwa Neema: ----------------------------------------------------------
7. Rhoda kwa Rehema: ----------------------------------------------------------
8. Hamisi kwa Daniela: ----------------------------------------------------------
9. Daniela kwa Rehema: ----------------------------------------------------------
10. Chifu Kariuki kwa Hamisi ----------------------------------------------------------
11. Bi. Kidude kwa Chifu Kariuki: ----------------------------------------------------------


## Kuandika

Look at each of the pictures and the summary of a description of each. Choose 2 pictures and write 10 sentences for each, describing the people in the pictures. Use complete sentences in each case as in the example given below.

**Maria**

1. Huyu ni Maria.
2. Maria anatoka Kenya.
3. Yeye ni Mkenya.
4. Ana umri wa **miaka minne**. (class 4)
5. Ana **nywele nyeusi** na macho rangi ya kahawia. (class 10)
6. Anavaa **rinda** la rangi ya waridi na zambarau. (class 5)
7. Anavaa **shati** ya rangi ya kijani kibichi. (class 9/10)
8. Anavaa **viatu** rangi ya zambarau. (class 7)
9. Maria anapenda mitindo na kustarehe.
10. Yeye hapendi kulala wala kula.

Jina: Maria
Nchi: Kenya
Uraia: Mkenya
Umri: 4
Nywele: Nyeusi
Macho: Kahawia
Rangi ya mavazi: rinda-waridi na zambarau ; blauzi-nyeupe
viatu: zambarau
Anapenda: mitindo; kustarehe
Hapendi: kulala, kula




Jina: Angie
Nchi: Turkey
Uraia: Mturuki
Umri: 9
Nywele: kahawia
Macho: Kahawia
Rangi ya mavazi:
rinda-nyekundu na manjano;
viatu-kijani kibichi
Anapenda: kuangalia televisheni; wanyama; vitabu
Hapendi: kupika, michezo



Jina: Harry
Nchi: Uingereza
Uraia: Mwingereza
Umri:18
Nywele: ndefu, nyeusi
Macho: bluu
Rangi ya mavazi:
shati- kijani kibichi;
suruali-nyeusi
Anapenda: kucheza gita, kuimba
Hapendi: kusoma, kula piza




Jina: Wang
Nchi: Uchina
Uraia: Mchina
Umri: 6
Nywele: fupi, nyeusi
Macho: kahawia
Rangi ya mavazi:
shati- bluu;
Suruali-bluu; viatu-vyekundu
Anapenda: filamu, kusafiri
Hapendi: kulala, kazi



**Kazi ya ziada**

**Rafiki mzuri**

1. Hapa chini, kuna sarafu zenye sifa za kuzingatia katika rafiki. Chagua sarafu nne zenye sifa zilizo muhimu zaidi kwako. Kata na ubandike sarafu hizo katika fremu ya picha.  Waonyeshe wengine picha yako! Waelezee ni kwa nini sifa hizi ni muhimu. Ona mfano (pdf file
https://www.jw.org/sw/mafundisho-biblia/watoto/mazoezi-ya-kujifunza/sifa-rafiki-mzuri/




2. Fikiria jinsi ambavyo utaonyesha sifa hizo nyumbani na kwa marafiki.

a) Juma la 1: Juma hili, nitafanyia kazi sifa ya ------------------------------------------------

Nitaionyesha kwa --------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------------

b) Juma la 2: Juma hili, nitafanyia kazi sifa ya ------------------------------------------------

Nitaionyesha kwa --------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------------

c) Juma la 3: Juma hili, nitafanyia kazi sifa ya ------------------------------------------------

Nitaionyesha kwa --------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------------

d) Juma la 4: Juma hili, nitafanyia kazi sifa ya ------------------------------------------------

Nitaionyesha kwa --------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------------

# KARIBU NYUMBANI

## Msamiati

### Sehemu za nyumba yetu

| Maelezo | Sehemu |
|---|---|
| Karibu nyumbani kwetu. Jihisi kuwa upo nyumbani. Hapa ni **mtaa** wa Nyayo. Ni mtaa safi na salama. Tumeishi hapa kwa miaka 12 sasa. Tunaupenda mtaa wetu sana kwani **majiran**i wetu ni **wazuri** na **hapana kelele**. Mimi na dada yangu mdogo tulizaliwa hapa. |  |
| Nyumba yetu si kubwa. Ina **sebule**, **jikoni** na **vyumba vitatu vya kulala**. Kwanza, hebu nikuonyeshe sehemu mbalimbali za nyumba yetu. Hii ni sebule. Sisi hukaa hapa jioni au wakati wa mapumziko. Pale nje, pana **baraza** na **bustani** ndogo **ya maua**. Tunapenda kupumzika katika veranda wakati ambao hali ya hewa ni nzuri badala ya kukaa hapa sebuleni. Nje pia kuna gereji ya kuegeshea gari. Baba huegesha gari lake katika gereji. |     |
| Hapa ni jikoni. Upande mmoja wa jikoni pana **friji na jiko**. Huu ni **mtungi wa gesi**. Upande huu mwingine pana **sinki.** Sisi huoshea vyombo hapa. **Hili kabati**. Katika hili kabati, kuna vyakula na katika kabati hili lingine, kuna vyombo kama sufuria, sahani, vikombe na vijiko. |   |

| | |
|---|---|
| Hii ni **bafu na msala**. Bafu ina maji lakini haina maji moto. Sisi hupashia maji ya kuogea jikoni kisha tunaweka kwenye **beseni la maji**. Vijijini, nyumba nyingi hazina bafu na misala ndani ya nyumba. Kwa kawaida, bafu na misala huwa nje ya nyumba. Pana sinki mbili bafuni. Unaweza kunawia mikono hapa na kupigia mswaki. |  |
| Hiki ni chumba cha mama na baba cha kulala. Ndani mna **kitanda** kikubwa, **meza na kiti**, na **televisheni** ndogo. Hawapendi tukiingia katika chumba chao cha kulala ovyo ovyo. |  |
| Hiki ni chumba changu na dada yangu. Katika upande mmoja pana kitanda changu na **kabati** langu **la nguo**. Katika upande huu mwingine pana kitanda cha dada yangu na kabati lake la nguo.Tuna **meza** moja tu hapa ndani kwa sababu chumba si kikubwa sana. Tunasomea na kufanyia kazi ya nyumbani hapa baada ya kutoka shuleni. |  |
| Hapa mwisho wa **ukumbi** pana **chumba cha wageni cha kulala**. Hapa ndipo utalala. Karibu ndani. Kitanda si kikubwa wala si kidogo sana. Ni cha upana wa wastani. Juu ya kitanda, pana **shuka** mbili, **blanketi** mbili **mito** miwili na **taulo** mbili. Utatumia meza hii unapofanya kazi yako. Utaweka nguo zako katika kabati hili. **Swichi ya taa ya umeme** ipo hapa karibu na mlango. |  |
| Mwisho, hakuna mahali pa kufulia nguo hapa ndani. Sisi hufulia nguo pale nje. Pana mfereji na kamba za kuanikia nguo. Pia, pana ndoo na beseni za kufulia nguo. Wakati mwingine, sisi hufulia nguo bafuni. Ninatumaini utafurahia kukaa nasi kwa wiki chache. Karibu. |  |

**Shughuli mbalimbali za nyumbani**

*kuoga* *kulala* *kupika* *kupumzika*
*kula* *kutazama televisheni* *kupiga mswaki* *kupanda maua*
*kupasha maji moto*

Mfano: kuegesha
**Tunaegesha** gari letu katika gereji.

| Sehemu ya nyumba | Shughuli |
|---|---|
| gereji | |
| sebule | |
| bafu | |
| baraza | |
| bustani | |
| jiko | |
| chumba cha kulala | |
| chumba cha maankuli | |

2. These are a few items/things found in or around the house. What are these items used for? You may list several things. See an example here below

| Item/thing | Activity |
|---|---|
| sinki | kunawia mikono, |
| kamba | |
| beseni | |
| meza | |

| | |
|---|---|
| jiko | |
| kabati | |

## Mazungumzo

### Majukumu ya nyumbani

Soma mazungumzo kisha ujibu maswali.

**Rhoda**: Sipendi siku ya Jumamosi kamwe. Nina shughuli nyingi sana.

**Jamaal**: Kwani wewe hufanya shughuli gani Jumamosi?

**Rhoda**: Mimi uamka asubuhi mapema kumsaidia mama na kazi jikoni.

**Jamaal**: Kazi gani Rhoda?

**Rhoda**: Kwanza, husaidia mama kupika kifungua kinywa. Kwa kawaida, sisi hutayarisha chai na mkata na hupika mayai.

**Jamaal**: Hiyo si kazi nyingi!

**Rhoda:** Sijamaliza. Baada ya kifungua kinywa, mimi na dada yangu Amina huosha vyombo na mama huenda sokoni.

**Jamaal:** Unafanya nini baada ya hapo?

**Rhoda:** Baada ya hapo, mimi husafisha nyumba na hufagia nje.

**Jamaal:** Kwani mkubwa wako Musa hasaidii na majukumu ya nyumbani?

**Rhoda**: Yeye husaidia lakini kazi yake mara nyingi ni kukata nyasi na kuosha gari la baba. Wakati mwingine yeye husaidia kusafisha bafu na kupanga makabati ya vitabu.

**Jamaal:** Dada yako huosha vyombo tu?

**Rhoda**: Hapana, mara nyingi husaidia mama kusafisha chumba chake cha kulala.

**Jamaal:** Eeh!

**Rhoda:** Sisi hufua nguo zetu kila Jumamosi. Mimi, dada na kaka yangu hufua nguo zetu na za wazazi wetu. Baadaye huzipiga pasi na huziweka kwenye kabati la nguo.

**Jamaal**: Baba yenu hufanya kazi yoyote?

**Rhoda:** Kwa kawaida yeye hufanya kazi Jumamosi. Unajua anafanya biashara na anahitaji pesa za kutulipia ada za shule. Jioni, yeye husaidia mfanyakazi wa shambani kulisha na kukamua ng'ombe.

**Jamaal**: Kwa kweli Jumamosi ni siku ya shughuli nyingi. Mimi huenda chuoni Jumamosi kwa hivyo sina majukumu mengi.

## Zoezi

Maswali

1. Familia ya Rhoda ina watu wangapi?
2. Familia ya Rhoda hula nini kwa kiamsha kinywa?
3. Nani katika familia hii huenda sokoni?
4. Baba anafanya kazi gani?
5. Jamaal hufanya nini Jumamosi?
6. Amina ana majukumu gani?

## Zoezi

Jibu maswali haya ya "kweli" au "si kweli"

| | kweli | sii kweli |
|---|---|---|
| 1. Mama husafisha chumba chake mwenyewe. | | |
| 2. Musa ni kaka mdogo wa Rhoda. | | |
| 3. Baba husaidia kukata nyasi. | | |
| 4. Musa ana dada wawili. | | |
| 5. Jamaal ni mwanafunzi. | | |
| 6. Amina husafisha chumba cha mama cha kulala. | | |

### Zoezi

Chora jedwali. Katika jedwali, andika majukumu ya nyumbani ya kila mtu katika familia yako. Pia, andika wakati majukumu haya yanafanywa.

| Nani? | Majukumu gani? | Wakati gani/saa ngapi? |
|---|---|---|
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |

# Kukodi nyumba

## Msamiati

Jifunze msamiati huu kisha ufanye mazoezi yanayofuata.

| | | | |
|---|---|---|---|
| nyumba ya kukodi | *rental house* | kupanga/kukodi | *rent (a place)* |
| ghorofa | *storey* | fanicha | *furniture* |
| malipo ya awali | *deposit* | kodi | *rent* |
| mtaa | *neighborhood* | mkataba | *contract* |
| mpangaji | *tenant* | mwenye nyumba | *landlord/lady* |
| wakala wa nyumba | *housing agent* | ulinzi/usalama | *security* |
| *kuhama* | *to move in/relocate* | eneo | *region* |

### Zoezi

Kamilisha sentensi hizi:

1. Mtu ambaye anakodi nyumba anaitwa …………………………………………………...
2. Nyumba ambayo ina ngazi ni nyumba ya ……………………………………………..
3. Pesa ambayo mpangaji hulipa kabla ya kuhamia nyumba ni ………………………
4. Pesa ambayo mpangaji hulipa kila mwezi ni …………………………………………
5. Mtu ambayu husaidia kutafuta nyumba anaitwa ……………………………………..
6. Mwenye nyumba na mpangaji huweka saini kwenye ………………………………..
7. Ulitoka nyumba moja na kwenda kuishi katika nyumba nyingine. Kwa hivyo ulifanya nini? …………………………………………

## Kusoma

### Tangazo la nyumba

Soma tangazo ambalo umepewa kisha ujibu maswali yanayofuata. Baadaye, utazungumza na mwanafunzi mwenzako kuhusu nyumba ambayo inawafaa zaidi.

Tangazo la 1

**Tangazo la nyumba ya kukodi**

Nyumba ya familia katika mtaa wa Kiserian, kilomita 22 kutoka jiji la Nairobi. Iko katika kiwanja cha ekari moja.

Nyumba hii ina ghorofa moja. Ina sebule mbili, jikoni na vyumba vitatu vya kulala. Ina bafu mbili. Nyumba haina fanicha yoyote.

Nyumba ina roshani kubwa upande wa chumba kikuu cha kulala. Nyumba ina umeme na jenereta na gereji ya magari mawili.

Nyumba hii iko karibu na bustani kubwa na maduka mengi. Barabara ni nzuri na kituo cha matatu kiko kama mita 100 kutoka nyumbani.

Kodi ya nyumba ni shilingi 40,000 au dola 400 kwa mwezi. Malipo ya awali ni dola shilingi 40,000. Utalipia umeme na maji.

Tangazo la 2

**Tangazo la nyumba ya kukodi**

Nyumba iko katika jengo la ghorofa la Tamaa katika mtaa wa Upper Hill. Jengo hili liko kilomita tatu tu kutoka jiji la Nairobi.

Nyumba iko katika ghorofa ya sita. Ina sebule, jikoni na vyumba viwili vya kulala. Ina fanicha katika kila chumba. Ina bafu moja. Kuna gereji katika ghorofa ya kwanza.

Kodi ya nyumba ni shilingi 65,000 au dola 650 kwa mwezi. Malipo ya awali ni dola shilingi 130,000 sawa na kodi ya miezi miwili. Utalipia umeme na ulinzi lakini mwenye nyumba atalipia maji na takataka.

Kweli au si kweli?

1. Nyumba ya Upper Hill iko karibu na jiji la Nairobi kuliko na nyumba ya Kiserian

2. Nyumba ya Kiserian ni ghali kuliko nyumba ya Upper Hill.
3. Mpangaji ambaye anaishi katika nyumba ya Kiserian hulipia umeme.
4. Nyumba zote mbili hazina fanicha.

## Zoezi

Katika majedwali haya, andika mambo ambayo unapenda na mambo ambayo hupendi kuhusu nyumba hizi mbili.

Nyumba ya Kiserian

| Ninapenda | Sipendi |
|---|---|
| | |

Nyumba ya Upper Hill

| Ninapenda | Sipendi |
|---|---|
| | |

# Mazungumzo

### Mazungumzo na wakala wa nyumba

Soma mazungumzo haya kati ya mpangaji na wakala wa nyumba kisha ujibu maswali yanayofuata:

**Mpangaji:** Hujambo? Ninatafuta nyumba ya kukodi.

**Wakala:** Sijambo. Ungependa nyumba katika mtaa gani?

**Mpangaji:** Katika mtaa wa Kiserian.

**Wakala:** Tuna nyumba nyingi katika mtaa wa Kiserian. Ungependa nyumba ya vyumba vingapi?

**Mpangaji: Nyumba ambayo ina** vyumba viwili vya kulala, sebule kubwa na jikoni kubwa.

**Wakala:** Tuna nyumba ambayo ina sebule na jikoni kubwa. Ina vyumba viwili vya kulala. Pia ina bafu mbili na misala miwili.

**Mpangaji:** Kodi ni pesa ngapi?

**Wakala:** Ni shilingi 35,000 kwa mwezi.

**Mpangaji:** Nitalipa malipo ya awali?

**Wakala:** Ndiyo: Malipo ya awali ni shilingi 35,000. Utalipa kodi ya mwezi mmoja na malipo ya awali kabla ya kuhamia katika nyumba hii.

**Mpangaji:** Kodi ni pamoja na huduma za maji na umeme?

**Wakala:** Hapana. Utalipia huduma za maji na umeme. Tutalipia huduma za ulinzi na kuondoa taka.

**Mpangaji:** Safi. Nitaweza kuona nyumba lini?

Wakala: Unaweza kuja kesho?

**Mpangaji:** Ndiyo. Nitakuja saa 2:30 mchana.

**Wakala:** Asante. Tutaonana kesho.

Maswali

1. Mpangaji angependa kuishi wapi?

2. Mpangaji anataka nyumba ya vyumba vingapi vya kulala?
3. Mpangaji atalipa pesa ngapi kwa jumla kabla ya kuhamia katika nyumba hii? Andika kwa maneno.
4. Kodi inajumuisha huduma za maji na umeme?
5. Mwenye nyumba hulipia huduma gani?
6. Mpangaji ataenda kuona nyumba lini na saa ngapi?

## Kusikiliza

Sikilizeni kwa makini mazungumzo haya kati ya mpangaji na mwenye nyumba. Jaza mapengo kisha ujibu maswali yanayofuata. Kisha jibu maswali yafuatayo.
Pata mazungumzo hapa: [https://mediaspace.illinois.edu/channel/channelid/95703161](https://mediaspace.illinois.edu/channel/channelid/95703161)

*Baraka looks for an apartment. He takes a tour of one house with a dalali.*

| | |
|---|---|
| DALALI: | Karibu sana Bwana Baraka. Jisikie nyumbani |
| Baraka: | Asante. Sijawahi kufika ……………………. hili la Arusha. |
| DALALI: | Kweli? Usa River ni ……………………. mzuri sana, utapenda. Kuna miti mingi, na mtaa huu ni ……………………. sana. Hakuna wizi. |
| BARAKA: | Safi sana. Usalama ni muhimu sana. Kuna askari anayekuja usiku? |
| DALALI: | Yupo kila siku. Bwana Baraka, wacha nikuonyeshe nyumba hii nzuri. Mwenyeji ……………………. bado, lakini wiki ijayo atatoka. |
| Baraka: | Sawa |
| DALALI: | Sasa tuko …………………….. Kuna nafasi kubwa hapa. Itafaa sana kwa familia. |
| Baraka: | Nikipanda ……………………. kuna nini? |
| DALALI: | Kuna jiko. Njoo tuangalie. |

*They walk upstairs to the kitchen*

DALALI: Sasa tuko ……………………, na tukiendelea mbele kuna bafu na ……………………..

Baraka: Sawa

DALALI: Mwishoni kuna …………………….

Baraka: Safi sana. Na vipi kuna …………………….?

DALALI: Ndiyo, familia moja inaishi kwa ghorofa ya juu, na mwanafunzi mmoja anaishi chini.

Baraka: ……………………. ya mwezi ni shilingi ngapi?

DALALI: Ni shilingi laki tano kwa mwezi.

Baraka: Mbona bei ghali?

DALALI: Nyumba hii inakuja na ……………………. na ulinzi. Ni bei nzuri tu.

Baraka: Kuna …………………….?

DALALI: Ndiyo, unatakiwa kulipa kodi ya miezi sita mwanzoni. ***Mkataba*** wa nyumba unaeleza kila kitu.

Baraka: Sawa, lakini Mzee, naomba upunguze bei kidogo. Fanya 450,000.

DALALI: Sawa nitazumgumza na ……………………. na kuona anasemaje.

Baraka: Haya, hebu nifikirie kama itanifaa, halafu nitakujulisha.

DALALI: Haya asante sana bwana

**Maswali**

1. User River ni mtaa mzuri kwa nini?
2. Nyumba hii ina vyumba vingapi vya kulala?
3. Askari wa User River huja kazini mara ngapi kwa wiki?
4. Mwenyeji atahama lini.
5. Jiko liko wapi katika nyumba hii?
6. Ni nani wengine wanaishi katika jengo hili?
7. Mpangaji (tenant) atalipa pesa ngapi kila mwezi?
8. Mpangaji atalipa kodi ya miezi mingapi kabla ya kuingia kwenye nyumba?

# SURA YA 4: VYAKULA NA MAPISHI

## Msamiati

### Vifaa vya jikoni

Draw simple pictures of the following items to demonstrate your understanding of what they are.

| Kiswahili | Kiingereza | Kiswahili | Kiingereza |
|---|---|---|---|
| sufuria | | mwiko | |
| jiko | | bakuli | |
| kifuniko | | sahani | |
| kikombe | | kijiko kikubwa | |
| kijiko cha chai | | kichungi | |

### Vitenzi maalum vya mapishi



-mimina



-katakata



-oka



-koroga



-chemsha



-kaanga



-changanya



-choma



-osha




-kanda



-menya



-pakua

## Sarufi na matumizi ya lugha

### Amri (Commands)

1. When making direct commands to one person, we use the verb root only. When we direct commands to more than one person, we drop the final vowel and add -eni to the verb root one  for one person. Look at these examples:

| Kwa mmoja (singular) | Kwa wawili au zaidi (plural) |
|---|---|
| Pika! | Pikeni! |
| Simama! | Simameni |
| Soma! | Someni! |
| Tembea! | Tembeeni! |
| Ruka! | Rukeni! |

2. To negate direct commands, we use ***usi-*** and ***msi-*** and add the subjunctive suffix ***-e*** at the end of the verb. Here are some examples.

| Kwa mmoja (singular) | Kwa wawili au zaidi (plural) |
|---|---|
| Usipike! | Msipike! |
| Usisimame! | Msisimame! |
| Usisome! | Msiome! |
| Usitembee! | Msitembee! |

Usiruke! Msiruke!

## Zoezi

*Andika amri kwa mtu mmoja kwa kutumia vitenzi hivi.*

1. Kupakua chakula ...............................................
2. Kuondoka hapa ...............................................
3. Kuenda jikoni ...............................................
4. Kusoma ...............................................
5. Kuondoka taka ...............................................
6. Kuangalia hapa ...............................................
7. Kusalimia mgeni ...............................................
8. Kufunga mlango ...............................................

## Zoezi

Andika amri kwa watu wawili au zaidi.

1. Kutenda wema ...............................................
2. Kula matunda ...............................................
3. Kufanya kazi ...............................................
4. Kusikiliza habari ...............................................
5. Kupakua mchuzi ...............................................
6. Kunywa ...............................................
7. Kuketi ...............................................
8. Kusafisha gari ...............................................

## Zoezi

Kanusha sentensi hizi (Write the following sentences in their negative form)

1. (Wewe) cheka. ...............................................
2. Tusome gazeti. ...............................................
3. Kimbieni. ...............................................
4. Waambie waje. ...............................................
5. Laleni sasa. ...............................................
6. Upike. ...............................................
7. Ni lazima waende shule. ...............................................
8. Wale chakula sasa. ...............................................

#### 4.3.2.2 Dhamira tegemezi (Subjunctive)

The subjunctive is used to express various ideas:

1. To ask for something

For example:

a) Tafadhali nipe maji.
b) Nisaidie na kitabu chako.

2. To recommend action

For example:

a) Ufanye kazi ya nyumbani kila siku. *Do your homework every day.*
b) Usisome kitabu hicho si kizuri. Don't read that book; it isn't good.

3. Doubt as to whether something will happen or not

For example:

a) Twende maktabani sasa? *Should we go to the library now (or not/or later)?*
b) Tuandike kitabu kweli? *Should we write a book really?*

4. To advise.

For example:

Heri uondoke sasa usichelewe. *It's better you leave now so that you're not late.*

Afadhali uenda hospitalini kama unaugua. *You better go to hospital if you're unwell.*

The subjunctive form

Practice is always recommended for mastery of grammatical forms. However, rules might help where you are not sure. Here are a few rules that you can learn so as to form the subjunctive accurately.

1. Use the same subject pronouns (viambishi awali) as you use in all other verbs. See the examples below
    a) <u>**Tu**</u>some
    b) <u>**Wa**</u>lipe
    c) <u>**A**</u>tembee

2. Do not use a tense marker. The subjunctive form does not show time-bound. Compare the tensed verbs and the subjunctives below:
    a) kitenzi cha kawaida: Tu<u>**na**</u>pika [wakati wa sasa]
       dhamira tegemezi: Tupike
    b) kitenzi cha kawaida: Wa<u>**li**</u>enda.
       dhamira tegemezi: Waende.

3. Drop the infinitive ku- in monosyllabic verbs.
    a) kula: Tule chakula
    b) kuja: Waje kesho
    c) kunywa: Mnywe kahawa

4) Drop the final vowel in verbs ending in ‘a’ and replace it with ‘e’. Look at the examples here:

| Kitenzi msingi | Mfano wa dhamira tegemezi |
|---|---|
| -pik**a** | Wapik**e** chai na mandazi. |
| -pand**a** | Tupand**e** basi. |
| -fik**a** | Wafik**e** saa ngapi? |
| -kat**a** | Ukat**e** tiketi mbili. |
| -pig**a** | Upig**e** simu jioni. |

5. Verbs ending in ‘e’ ‘i’ au ‘u’, do not change. For example:

| Kitenzi msingi | Mfano wa dhamira tegemezi |
|---|---|
| -faham**u** | Wafaham**u** maana ya methali hizi. |
| -jaribu | Ujarib**u** kufika mapema. |
| -fikir**i** | Tufikir**i** kuhusu jambo hilo. |
| -ajir**i** | Mwajir**i** mtoto wangu tafadhali. |
| -sameh**e** | Msameh**e**. |

6. Negation

To negate the subjunctive, infix “-si-” between the subject marker and the root verb.

a) U**si**ende leo.
b) Watoto wa**si**nywe maji baridi.
c) M**si**jaribu kuruka kwenye maji.
d) Huyu kijana ni mvivu sana. U**si**mwajiri.
e) U**si**chelewe.

7. When directly addressing more than one person, -ni is suffixed to the subjunctive verb. For example:

a. **Twendeni** chuoni.
b. **Fungueni** vitabu vyenu.
c. **Pikeni** wali na nyama.
d. **Njooni** kesho jioni.

8. There are certain words such as the ones here below that commonly trigger the subjunctive.

-ambia-tell

afadhali-it's better (to do something)

ni lazima- it's a must

inabidi- have to

ni vyema-it's good (to do something)

Ili-so that

For example:

| | |
|---|---|
| 1. **Waambie wacheze** ngoma. | *Tell them to play the drums.* |
| *2.* **Ni lazima ufunge** mlango. | *You must close the door.* |
| *3.* **Afadhali tuende** Chicago. | *It's better we go to Chicago* |
| 4. **Inabidi nilale** sasa. | *I have to sleep now* |
| *5.* Tuondoke sasa **ili tufike** mapema. | *Let's leave now so that we arrive early.* |

## Kusoma

### Vyakula vya Afrika Mashariki

Soma maelezo haya kisha ujibu maswali ya ufahamu yanayofuata. Baadaye, utajadili masuala kadhaa kuhusu vyakula na wanafunzi wenzako.

| | |
|---|---|
|   | Kwa vile kuna makabila mengi katika Afrika Mashariki, navyo vyakula ni vya aina tofauti katika sehemu hizi. Aina hizi hulingana na eneo wanakoishi watu. Kwa mfano, watu wanaoishi karibu na maziwa au bahari hula samaki kwa wingi. Watu wanaofuga wanyama hupenda kula nyama.  Hapa, utasoma kuhusu vyakula wanavyovipenda watu wa Afrika ya Mashariki. |
|   | Watu wengi wanapenda kunywa chai asubuhi na jioni. Watu hunywa chai moto yenye maziwa na sukari. Kwa kawaida, kwa wageni kukaribishwa kwa chai kabla ya kupewa chakula. Hii ni njia moja ya kuonyesha ukarimu. |
|     | Kwa kawaida, watu wengi hawali chakula kizito asubuhi. Watu wengi hunywa chai na mkate kwa chakula cha asubuhi. Wengine hupenda kunywa chai na viazi vitamu au mayai. Mara kwa mara, watu hunywa chai na mandazi au chapati na chai asubuhi. |
|   | Vyakula vya mchana na jioni huwa vizito kuliko vyakula cha asubuhi. Kwa mfano, baadhi ya watu hula wali na mchuzi wa nyama au maharage wakati wa mchana na ugali na sukumawiki wakati wa jioni. Ugali ni chakula maarufu sana. Watu hula ugali na mchuzi wa nyama, kuku au samaki. Wakati mwingine, |

| | |
|---|---|
|   | baadhi ya watu hula ugali na nyama choma na kachumbari. |
|   | Baadhi ya vyakula kama pilau, chapati na biriani huliwa na watu wa bara sana sana wakati wa sherehe. Lakini hivi ni vyakula vinavyoliwa na watu wa pwani wakati wowote. Pilau na biriani ni wali uliopikwa kwa viungo kama mdalasini, kitunguu saumu, tangawizi, bizari na karafuu. |
|   | Watu wengi hawapendi vyakula ambavyo havijapikwa kama saladi na sandwichi. Kwa kuwa chakula cha mkahawa ni bei ghali, watu wengi hupenda kula chakula nyumbani. |

## Zoezi

Kweli au si kweli?

| Sentensi | kweli | si kweli |
|---|---|---|
| 1. Vyakula vya asubuhi ni vizito kuliko vyakula vya jioni. | | |
| 2. Watu wengi hunywa chai yenye maziwa. | | |

| | | |
|---|---|---|
| 3. Baadhi ya watu hula ugali na maharage | | |
| 4. Chapati na biriani huliwa watu wa pwani wakati wowote | | |
| 5. Watu wengi hula wali na mchuzi wa nyama au maharage kwa chakula cha mchana | | |

## Hoteli ninayoipenda

**Hoteli ya Mt. Meru**

Hoteli ya Mt. Meru ipo miguuni ya Mlima Meru jijini Arusha. Hoteli hii ina mikahawa minne. Hapa, utapata vyakula vya kimataifa kutoka nchi mbalimbali. Pia, tuna aina nyingi za mvinyo, juizi na pombe. Unataka kiamsha kinywa? Usiende mbali. Hapa hotelini, utapata kiamsha kinywa aina ya “continental”. Pia, utapata chakula cha mchana aina ya “buffet’ na cha jioni kwa bei nafuu.

Hoteli ina aina ya malazi yanayofaa msafiri yeyote. Bali na kuwa na vyumba vyenye kitanda kimoja, tuna vyumba vyenye vitanda viwili, “Executive suites”, na vyumba vinavyowafaa walemavu. Kila chumba kina televisheni, simu, WIFI ya malipo, maikrowevu na friji ndogo. Pia kina mashine ya kutengenezea kahawa au chai.

Ukikaa katika hoteli yetu, utafurahia ukarimu wetu na huduma bora. Mpokezi wetu atakukaribisha unapofika na wafanyi kazi wetu watahakikisha chumba chako ni safi. Utaweza kutumia huduma zetu katika kituo kidogo cha biashara, kuogelea katika bwawa letu la kuogelea ambalo lina sehemu ya watoto. Pia, utapata maegesho bila malipo.

Maoni ya watu 244 waliokaa katika hoteli yetu wameipa pointi za ubora 4.3 kwa tano kwenye maoni ya Google.

**Hotel ya Gold Crest , Arusha**

Hoteli ya Gold Crest iko katika barabara ya Old Moshi, kilomita moja kutoka katikati ya jiji la Arusha. Kutoka hapa, uataweza kusafiri sehemu mablimbali kama Ngorongoro Crater, Serengeti na Mt. Meru kwa urahisi.

Hoteli yetu ina ukumbi wa kufanyia mazoezi, bwawa la kuogelea, maegesho bila malipo na WIFI bila malipo. Tuna vyumba aina mbalimbali kulingana na mahitaji ya wateja wetu. Tuna chumba cha “Single Executive”, “Double Executive Suite” na “Family Suite”. “Family Suite” ina sebule, sofa na viti. Pia, ina friji na maikrowevu.

Kila chumba kina televisheni na simu. Utapata huduma za dobi za haraka ukizihitaji. Pia, tuna huduma za usafiri kutoka uwanja wa ndege wa kimataifa wa Julius K. Nyerere.

Tuna kituo kidogo cha biashara ambacho hufunguliwa kwa saa 24. Pia, kila chumba kina huduma za usalama za CCTV.

Vyakula ni vya aina ya halal. Utapata kiamsha kinywa bila malipo. Pia, tuna baa ya mvinyo ambapo utaweza kupumzika wakati wowote kutoka saa saba hadi saa tano usiku.

Wateja wetu 59 wameipa hoteli hii pointi 3.8 kwa 5 za ubora kwenye Google Reviews.

| **Mt Meru** | | **Gold Crest** | |
|---|---|---|---|
| **Faida** | **Hasara** | **Faida** | **Hasara** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |

## Mazungumzo

### Mkahawani

**Mhudumu:** Habari za alasiri? Nikusaidie na kinywaji?

**Mteja:** Ndiyo. Tafadhali nisaidie na maji moto na kipande cha ndimu.

**Mhudumu:** Ungependa kula chochote kabla chakula chako kiwe tayari?

**Mteja:** Kama nini?

**Mhudumu:** Samosa, mshikaki au soseji.

**Mteja:** Ndiyo. Tafadhali nipe samosa mbili za nyama.

**Mhudumu:** Na chakula je? Ungependa kuagiza nini?

**Mteja:** Ningependa kuku iliyochomwa, wali wa nazi, chapati na sukuma wiki.

**Mhudumu:** Ungependa supu?

**Mteja:** Bila shaka. Nipe bakuli moja ya supu.

**Mhudumu:** Sawa. Nipe dakika chache nitakuletea kinywaji na samosa. Chakula kitakua tayari baada ya dakika kumi hivi.

*Baada ya dakika chache*

**Mhudumu:** Chakula kilikuwa kizuri?

**Mteja:** Nimekifurahia sana, asante.

**Mhudumu:** Safi. Ndiyo hii bili yako.

**Mteja:** Asante sana? Mnachukua kadi?

**Mhudumu:** Hapana. Utalipa pesa taslimu.

**Mteja:** Hamna shida. Hizi hapa shilingi elfu mbili.

**Mhudumu:** Nitakupa cheji ya shilingi mia mbili sabini na tano.

**Mteja:** Asante.


**Mhudumu:** Karibu tena.

# SAFARI

## Msamiati

1. Oanisha maneno na picha.

| Picha | Jina |
|---|---|
| 1. pasi ya usafiri [n/n] |   |
| 2. mizigo [m/mi] |  |
| 3. uwanja wa ndege |  |
| 4. hoteli [n/n] |   |

| | |
|---|---|
| 5. mtalii [m/wa] |   |
| 6. tiketi [n/n] |   |
| 7. shilingi [n/n] |   |
| 8. ramani [n/n] |  |
| 9. viza [n/n] |   |

## Zoezi

Tumia **msamiati 1-9** kukamilisha sentensi hizi. Tumia kila neno mara moja tu.

1. Ninasoma katika Chuo Kikuu cha Illinois. Kwa hivyo, mimi ni mwanafunzi sio ……………………………....
2. Mimi na kaka yangu tutaenda Tanzania. Kwa hivyo nitanunua …………………….. mbili za ndege.
3. Nitalipia tiketi kwa dola wala sio …………………………….....
4. Nitahitaji …………………………….... na …………………………….... kuingia nchini Tanzania.
5. Nitalala katika …………………………….. ya Hilton.
6. Nitabeba …………………………….. michache.
7. Ndege itaondoka kutoka …………………………….. wa O'Hare.
8. Nitanunua …………………………….. ya mji wa Dar es Salaam nitakapofika.

## Sarufi

**Conditional -nge- na -ngali-**

There are various ways of expressing "condition" or "probability" in Swahili. The conditional mood helps express these two ideas. They are expressed by various markers. In this section, we will focus on the two markers of conditional mood, *-nge-* and *-ngali-.*

**Conditional *-nge-***

This is marked by *-nge-* in affirmative sentences and *-si-nge-* in the negative [if + simple past tense...would]. This refers to a condition that could hypothetically be fulfilled in the present, i.e if one condition is met now, it would result in the fulfilment of something/ wish.

Mifano:

U**nge**enda harusi, u**nge**mwona Alicia. *If you went to the wedding, you would*

| | |
|---|---|
| | *have seen Alicia.* |
| U**singe**enda harusi, u**singe**mwona Alicia | *If you did not go to the wedding you would not see Alicia* |
| Tu**nge**soma, u**nge**faulu. | *If we studied, we would succeed.* |
| Tu**singe**soma, u**singe**faulu. | *If we did not study, we would not succeed.* |
| Wa**nge**safiri leo, wa**nge**fika kesho. | *If they travelled today, they would arrive tomorrow.* |
| Wa**singe**safiri leo, wa**singe**fika kesho | *If they did not travel today, they would not arrive tomorrow.* |

**Conditional *-ngali-***

Another type of conditional mood is one that refers to an unrealistic condition which could have been fulfilled in the past. It expressed by *-ngali-* [ *-ngali-* + *past perfect* … *would have*] in the affirmative and -*si-ngali-* in the negative. See the examples below:

1. U**ngali**enda harusi, u**ngali**mwona Alicia. *If you had gone went to the wedding, you would have seen Alicia.*
2. U**singali**enda harusi, u**singali**mwona Alicia. *If you had gone to the wedding you would not have seen Alicia.*
3. Tu**ngali**soma, tu**ngali**faulu. *If we had studied, we would have succeeded.*
4. Tu**singali**soma, tu**singali**faulu. *If we had not studied, we would not succeeded.*
5. Wa**ngali**safiri leo, wa**ngali**fika kesho. *If they had travelled today, they would have arrive tomorrow.*

The conditional -nge- and -ngali- is often used to express the notion of “would” and “would have”

| | |
|---|---|
| Ningependa | *I would like* |
| Nisingependa | *I would not like* |
| Ningalipenda | *I would have liked* |
| *Nisingalipenda* | *I would not have liked* |

## Zoezi

*1. Tafsiri*

a) We would leave

b) They would buy a ticket

c) She would have called

d) He would not pay

e) I would not have paid

f) You would say

g) They would have boarded the bus

h) I would visit

*2. Kanusha sentensi hizi.*

a) Ningependa kununua tiketi ya ndege

b) Ungetaka kwenda tarehe gani?

c) Ningetaka kusafiri tarehe 25 mwezi wa Julai.

d) Ningependa kuondoka kutoka uwanja wa ndege wa O'Hare, mjini Chicago.

e) Ningependa kuondoka jioni.

f) Ningependa kusafiri kwa Delta Airlines.

## Kusoma

### Safari ya Alex nchini Kenya

Soma fungu hili fupi kuhusu safari ya Alex nchini Kenya. Unaposoma, jibu maswali haya:

1. Kwa nini Alex alibeba jakezi nzito na sweta?
2. Alex ametembelea Kenya mara ngapi?
3. Alex alifanya mambo matatu muhimu kabla ya kusafiri. Ni mambo gani hayo?
4. Alipataje chumba cha kulala?
5. Alex alifanya nini alipokuwa safarini?
6. Alex alifika katika uwanja gani wa ndege?
7. Kwa nini Alex na Peter walisimama njiani?

Alex atatembelea Kenya msimu wa baridi mwaka uliopita. Atafika Nairobi katikati ya mwezi wa Juni. Hali ya hewa itakuwa baridi sana kwa hivyo, **atabeba** mavazi mengi ya baridi kama vile jaketi nzito, sweta, buti, kofia na skafu. Pia, kwa sababu yeye huugua ugonjwa wa pumu, ataleta dawa zake.

Itakuwa mara yake ya kwanza kutembelea Kenya. Atahitaji pasi ya usafiri na viza. Pia atahitaji kununua tiketi ya ndege. Kabla ya **kuondoka**, Alex ataenda katika ubalozi wa Kenya ili kupata viza. Pia, atanunua tiketi moja ya ndege na kupata chumba cha kulala katika hoteli moja nchini. Labda ataweza kupata chumba na tiketi ya bei rahisi katika tovuti ya *Tripadvisor.* Kwa sababu safari itakuwa ndefu, Alex atasoma vitabu na kusikiliza muziki kwenye simu yake atakapokuwa safarini. Ninatumaini hatasahau kubeba chanja yake ya simu. Kama ataisahau, hataweza kusikiliza muziki kwa muda mrefu.

Rafiki yake Peter atamchukua kutoka uwanja wa ndege wa kimataifa wa Jomo Kenyatta. Peter atamsaidia kuweka mizigo yake kwenye gari. Pia atamsaidia kubalilisha pesa. Atahitaji kubadilisha dola kwa shilingi. Ataweza kubalisha katika mojawapo ya benki katika uwanja wa ndege. Njiani, watanunua chakula. Kisha wataendelea na safari hadi hotelini.

## Kusikiliza

### Tiketi ya ndege

Jifunze msamiati huu wa usafiri

| Kiswahili | Tafsiri |
|---|---|
| safari (n) | trip |
| wakala wa usafiri (n) | travel agent |
| barua pepe (n) | email |
| uwanja wa ndege wa kimataifa (n) | international airport |
| bei | price/cost |
| -safiri (v) | travel |
| -ondoka (v) | leave |
| -fika (v) | arrive |
| -rejea (v) | return |
| -kata tiketi | buy a ticket |
| shirika la ndege | airline |

Jaza mapengo katika sentensi hizi na maneno mwafaka kutoka kwa jedwali la msamiati hapo juu.

1. Dada yangu ……………………………….. nyumbani jana.

2. Nitaenda Honolulu mwezi ujao kwa hivyo ………………………………..ya ndege.
3. Nani ataenda ……………………………….. Afrika Mashariki mwaka kesho?
4. ……………………………….. ya tiketi za ndege ni ghali sana.
5. Nitasafiri kutoka ……………………………….. wa O'Hare.
6. Rafiki yangu alienda Uchina lakini ……………………………….. hapa nchini kesho.
7. Nitanunua tiketi yangu ya ndege kutoka kwa ………………………………...

## Mazungumzo

### Kubadilisha ratiba ya usafiri

Alex angependa kubadilisha ratiba yao ya usafiri. Anapigia wakala wa usafiri simu. Soma mazungumzo yao kisha ujibu maswali yanayofuata.

**Msamiati muhimu**

| | |
|---|---|
| ratiba | *schedule* |
| kufanya mabadiliko | *to make changes* |
| -kata tiketi | *buy a ticket* |
| kubadilisha | *to change* |
| machache | (a)*few* |
| kutua | *to land* |
| bado | *still* |
| badala ya | *instead of* |
| hamna shida | *no problem* |
| jambo | *issue* |

**Wakala wa usafiri**: Hujambo?

**Alex:** Sijambo.

**Wakala wa usafiri:** Nikusaidie na nini?

**Alex.** Nilikata tiketi mbili za ndege lakini ningependa **kufanya mabadiliko machache.**

**Wakala wa usafiri: Ulikata tiketi** lini?

**Alex:** Jana.

**Wakala wa usafiri:** Sawa. Tunaweza kubadilisha.

**Alex: Badala ya** kusafiri tarehe 25 mwezi wa Julai, tungependa kusafiri tarehe 12 mwezi wa Agosti.

**Wakala wa usafiri:** Sawa. Kuna jambo lingine?

**Alex:** Pia, tungependa **kutua** katika uwanja wa kimataifa wa Moi mjini Mombasa badala ya uwanja wa kimataifa wa Jomo Kenyatta.

**Wakala wa usafiri:** Mngependa kuondoka usiku **bado**?

**Alex:** Ndiyo.

**Wakala wa usafiri: Hamna shida**. Nitatafuta tiketi sasa hivi..

**Alex:** Asante.

**Maswali**

a) Kwa nini Alex anapigia wakala wa usafiri simu?
b) Baada ya kufanya mabadiliko, Alex na Joy watasafiri tarehe gani?
c) Baada ya kufanya mabadiliko, Alex na Joy watatua wapi?
d) Kabla ya kufanya mabadiliko, Alex na Joy angetua wapi?
e) Baada ya kufanya mabadiliko, Alex na Joy wataondoka wakati gani?

## Kusikiliza

Alex anataka kusafiri na mpenzi wake Joy. Kabla ya kwenda, Alex **anapigia** wakala wa usafiri **simu** ili anunue tiketi. Sikiliza mazungumzo haya baina ya Alex na wakala wa usafirI. Unaposikiliza, jaza mapengo katika mazungumzo haya. {media space link}

Baada ya kusikiliza, jaza jedwali hili na taarifa mwafaka kutoka katika mazungumzo haya.

| | |
|---|---|
| majina ya wasafiri | |
| tarehe ya kusafiri | |
| bei ya tiketi mbili | |
| shirika la ndege | |
| kuondoka kutoka | |
| saa ya wasafiri kuondoka | |
| saa ya wasafiri kufika | |

Haya ni mazungumzo kati yako na wakala wa usafiri. Jaza mapengo na msamiati mwafaka.

**Wakala** Hujambo?

Wewe**:** Sijambo.

**Wakala:** ………………………………..?

**Wewe.** Nilikata tiketi moja ya ndege lakini ningependa kufanya

………………………………..

**Wakala:** Ulikata ……………………………….. lini?

**Wewe:** Juzi. Alhamisi.

**Wakala:** ……………………………….. kufanya mabadiliko gani?

**Wewe:** ……………………………….. kusafiri tarehe 3 mwezi wa Desemba, ningependa ……………………………….. kusafiri kati ya tarehe 6 na tarehe 15 mwezi wa Machi.

**Wakala:** Sawa. Kuna jambo lingine?

**Wewe:** Pia, tungependa ……………………………….. katika uwanja wa kimataifa wa Dar es Salaam badala ya uwanja wa Kilimanjaro.

**Wakala:** Ungependa kuondoka ………………………………..

**Wewe:** Kati ya saa mbili na saa tano usiku.

**Wakala:** ………………………………...

**Wewe:** Asante sana.

## Kusoma

**Karibu pwani**

Nilifika hapa jana usiku. Awali, nilitembelea mji wa Mombasa lakini sikuweza kwenda ufukweni. Watu wengi husema kuwa hawajaona fukwe safi na zenye mchanga safi na mweupe kama fukwe za Mombasa. Kwa hivyo, nilifunga safari ya Mombasa ili nijionee mwenyewe. Nipo hapa ufukweni wa Bamburi. Mbali na ufukwe wa Bamburi, kuna fukwe nyingi hapa pwani kama vile Nyali, Diani, Shanzu na Tiwi. Bahari ya Hindi inaenea mbali kutoka fukwe hizi. Ninajaribu kutupa macho yangu nione mwisho wa bahari lakini siuoni mwisho wake.

Ufuoni wa bahari, ninaona watu wengi wanaotembea hapa na pale. Kuna watalii na wenyeji. Watalii wana furaha labda kwa sababu hali ya hewa ni nzuri sana leo. Hakuna joto jingi kama kawaida. Kuna upepo mwanana kutoka baharini.

Watu wengi wanaogelea baharini. Wengine wanapumzika kwenye vitanda vya baharini chini ya miavuli. Baharini, kuna watelezaji mawimbi pia na unaweza kusikia sauti ya mashua na mawimbi. Watoto wanakimbizana huku na kule. Wanashindana kuokota makombe ya baharini.





Ukingoni wa bahari kuna minazi mirefu. Pia kuna mikahawa ya kifahari kama vile Sarova White Sands na. Mbali kidogo, kuna nyumba za makuti. Ninaelewa kuwa ni kawaida kuona nyumba za makuti hapa pwani. Watu hujenga nyumba zao kwa makuti kwa ajili ya kujikinga na joto jingi. Hali ya joto hapa pwani huwa juu sana.



minazi




nyumba ya makuti

Hapa, biashara ni za aina tofauti. Wachuuzi wanatembea tembea wakizungumza na kuuza bidhaa za kumbukumbu. Kama shuka za Wamaasai, vikapu, vinyago na shanga. Wachuzi hupenda kuuzia watalii kutoka nchi za ughaibuni kwa sababu wao hununua bidhaa hizi kwa bei nzuri. Kuna watu ambao wanawa beba watalii kwa ngamia. Watalii wanalipa pesa kidogo kwa “safari” hizi fupi za ngamia.



Safari yangu ilikuwa tofauti na safari ya hapo awali. Leo tulisafiri kwa treni ya Madaraka Express kutoka kituo cha Treni cha Syokimau, Nairobi, karibu na

uwanja wa kimataifa wa Jomo Kenyatta. Safari ya treni huchukua saa 5 hadi kituo cha treni cha Miritini mjini Mombasa. Awali, safari ya treni ilichukua saa 15 na kwa hiyo, wasafiri wengi walipendelea usafiri wa basi au gari binafsi.

Treni za Madaraka Express hupitia katika mbuga ya wanyama ya Tsavo. Hii ni mbuga ambayo ina wanyama wengi wa porini. Wasafiri walifurahi kuona ndovu, punda milia, na swara. Mzee mmoja alisema kuwa katika safari yake ya awali aliona simba. Kuna nyati pia lakini hatukuwaona.

Maswali



1. Kwa nini mwandishi alifunga safari kwenda Mombasa?
2. Mwandishi alisafirije kwenda Mombasa?
3. Kwa nini wachuuzi wanapenda kuuzia watalii wa ughaibuni bidhaa zao?
4. Mwandishi aliona wanyama gani katika mbuga ya wanyama ya Tsavo?
5. Mwandishi anafikiri watalii wana furaha kwa nini?
6. Kwa nini watu wa pwani hujenga nyumba za makuti?
7. Nauli ya treni ni pesa ngapi?


Kweli au si kweli?

1. Mwandishi anakaa katika hoteli ya Bamburi.
2. Kabla ya kwenda Mombasa, mwandishi alienda kutembelea mbuga ya wanyama ya Tsavo.
3. Mwandishi hajatembelea ufukwe wa Bamburi hapo awali.
4. Safari ya treni kutoka Nairobi hadi Mombasa huchukua saa 15.
5. Wasafiri wengi wanapendelea usafiri wa basi au gari binafsi.

## MJINI

Alex na Joy walipokuwa Nairobi, walizuru sehemu mbalimbali za mji. Picha hizi zinaonyesha mahali walipotembelea. Oanisha picha na msamiati.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. mkahawa | a.  | 2. makavazi | b.  |
| 3. mbuga ya wanyama | d.   | 4. uwanja wa michezo | e.  |
| 5.maktaba | f.  | 6. maduka makubwa | g.   |
| 7. benki | h.  | 8. kituo cha zima-moto | i.  |
| 9. posta | j.  | 10. jengo la bunge | k.   |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 11. duka la dawa | l.  | 12. ukumbi wa mazoezi | m.  |
| 13. supamaketi | n.  | 14. ukumbi wa sinema | o.  |
| 15. bustani | p.  | 16. hospitali | q.  |
| 17. kituo cha basi | r.  | 18. kituo cha polisi | s.  |

## Sarufi na matumizi ya lugha

The verb to have (kuwa na)

a) Mahali huku …………………………….. uchafu kwa hivyo sitaki kukaa huku.

b) Nchi ya Tanzania …………………………….  mashariki ya Afrika.

c) Maeneo mengi ya Afrika Mashariki …………………………….  joto nyusi ya wastani.

d) Milima michache ya Afrika Mashariki ……………………………. na theluji kileleni.

e) Barabara nyingi za lami Afrika Mashariki ……………………………. mitaani sio mashambani.

f) Kisiwa cha Pemba ……………………………. kusini ya kisiwa cha Zanzibar.


g) Ufuko wa Diani ……………………………. katika pwani ya Mombasa.

h) Viwanja vya ndege vya kimataifa vya Moi na Kenyatta ……………………………. nchini Kenya.

## Dira

Angalia dira iliyo hapa chini na uonyeshe mishale yake inaelekea wapi.

| | | |
|---|---|---|
| magharibi | kusini magharibi | kaskazini magharibi |
| mashariki | kaskazini mashariki | kusini mashariki |
| kusini | kazkazini | |



## Zoezi

Angalia ramani hii ya mji na ufanye zoezi hili la 2.




Tumia vihusishi vinavyofaa katika orodha hii kujibu maswali katika zoezi hili.

| | | |
|---|---|---|
| mbele ya | nyuma ya | karibu na |
| kushoto mwa | kaskazini mwa | kaskazini mashariki mwa |
| kaskazini magharibi mwa | kusini magharibi mwa | kusini mashariki mwa |
| magharibi mwa | mashariki mwa | upande wa kushoto wa |
| kando ya | upande wa kulia wa | pembeni mwa |

1. Hoteli iko wapi kutoka kituo cha zima-moto?
2. Benki iko wapi kutoka bustani?

3. Posta iko wapi kutoka maktaba?
4. Duka la dawa liko wapi kutoka posta?
5. Maduka yako wapi kutoka benki kuu?
6. Makavazi yako wapi kutoka hospitalini?

## Kusoma

### Usafiri mjini

Msamiati

| | | | |
|---|---|---|---|
| njia ya usafiri | kondakta wa daladala | kuchukua | |
| kupanda | pikipiki | usafiri wa umma | nauli |

*Baada ya kukaa nchini Kenya kwa wiki chache, Joy na Alex walienda Arusha, Tanzania. Endelea kusoma juu ya safari ya Joy na Alex.*

Joy na Alex waliondoka kutoka uwanja wa ndege wa kimataifa wa Kenyatta saa kumi jioni. Waliwasili katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Kilimanjaro karibu saa kumi na moja jioni.  Kutoka uwanja wa ndege, walichukua teksi hadi mjini Arusha. Safari ya gari kutoka Uwanja wa ndege wa kimataifa wa Kilimanjaro hadi Arusha ni ndefu. Walipofika mjini, walishangaa kuona idadi kubwa sana ya watu na magari. Kwanza walihitaji kwenda hotelini lakini hawakujua ni njia gani ya usafiri bora kwenda hotelini. Walisimama kando ya barabara. Hawakujua kama wavuke barabara au waelekee upande wa kushoto au wa kulia.  Walisimama pale kwa muda mrefu.



Ghafla, walisikia sauti. “Njiro, Njiro, twende Njiro,” kondakta wa daladala akasema. Alex na Joy walimwangalia tu. Hawakujua kwamba walihitaji kupanda kwenda hotelini. Wangechukua teksi lakini bei ya teksi ni ghali mno. Waliendelea kusimama pale. Palikuwa na kelele nyingi ya daladala na pikipiki.

Mjini Arusha, wasafiri wengi hutumia daladala au pikipiki kusafiri kutoka mjini kwenda mitaani. Ndani ya mji, watu wengi huenda sehemu mbalimbali za mji kwa miguu. Wasafiri wanaoenda katika miji mingine husafiri kwa basi kutoka Arusha. Mabasi huondoka kutoka kituo cha basi cha Kilombero kila siku kuenda miji kama Babati, Dodoma na Singida.



*usafiri wa basi*



*usafiri kwa pikipiki*

Baada ya kusimama pale kwa muda mrefu, waliamua kuchukua teksi hadi hoteli ya Impala. Nauli ilikuwa shilingi 28,000. Wangesafiri kwa daladala, labda wangelipa shilingi 1,500.

Maswali

a) Alex na Joy walisafirije kutoka Nairobi?
b) Walisafirije kutoka uwanja wa ndege wa Kilimanjaro?
c) Angalia maana ya “usafiri wa umma”. Toa mifano miwili ya usafiri wa umma mjini Arusha.
d) Alex na Joy walisafirije kwenda hotelini?

e) Wasafiri wengi mjini Arusha hutumia njia gani ya usafiri?

f) Wasafiri wanaoondoka kutoka Arusha kwenda miji mingine hutumia njia gani ya usafiri?

## Mazungumzo

Simba is lost. He calls his friend Nafisa to ask him how to get to the hotel from the park. Read the conversation below then answer the questions that follow.

**Simba:** Hujambo Nafisa?

**Nafisa:** Sijambo Nafisa. Habari za mchana?

**Simba:** Nzuri sana lakini nimepotea. Ninataka kwenda hotelini.

**Nafisa:** Uko wapi?

**Simba:** Katika bustani. Hoteli *iko mbali kutoka hapa*?

**Nafisa:** Hapana. Si mbali sana. Ni kilomita mbili hivi.

**Simba:** *Nitaendaje?*

**Nafisa:** Kutoka bustani, *elekea kaskazini* na *uingie kwenye barabara* ya Kigali. Utaona makavazi *kaskazini mwa* barabara ya Kigali. *Pinda kushoto* katika barabara ya Kigali. *Nenda moja kwa moja* hadi makutano ya barabara ya Kigali na barabara ya Moshi.

**Simba:** Nikifika makutano, *nipinde kushoto au kulia?*

**Nafisa:** *Usipinde. Endelea mbele.* Utaona hoteli *upande* wako *wa kulia.* Pita na *uende hadi makutano* ya barabara ya Kigali na barabara ya Kampala. *Pinda kulia*. Utaona lango kubwa la hoteli *upande* wako *wa kulia*.

Jibu maswali haya:

1. Simba anataka kwenda wapi?
2. Simba anatoka wapi?
3. Kutoka bustanini hadi hotelini ni maili ngapi?
4. Simba akifika katika barabara ya Kigali atapinda kushoto au kulia?
5. Simba akifika makutano ya ya barabara ya Kigali na barabara ya Moshi, *a*tapinda

Wapi?








6. Makavazi yako wapi kutoka bustani?

7. Hoteli iko upande gani wa bustani?

# MANUNUZI

## Msamiati

Andika majina ya mavazi haya

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1.  | 2.  | 3.  | 4.  |
| 5.  | 6.  | 7.  | 8.  |
| 9.  | 10.  | 11.  | 12.  |
| 13.  | 14.  | 15.  | 16.  |

## Sarufi na matumizi ya lugha

Making requests

The process of buying things involves making requests. There are some common ways of making requests. They are stated here below.

1. Asking a question

    (i) Je, unaweza kunitembelea wiki ijayo?

    (ii) Unaweza kunipeleka mjini?

    (iii) Je, unaweza kuninunulia matunda?

2. Stating a request

In stating a request, the verb “omba” is commonly used.

(i) Ninaomba kalamu.

(ii) Ninaomba nguo safi.

(iii) Tunaomba gari lako.

3. Command and the word “tafadhali”

(i) Ongeza kidogo, tafadhali.

(ii) Punguza bei, tafadhali.

(iii) Nipe unga wa ngano, tafadhali

## Zoezi

1. You are at a restaurant. Order a meal of your choice.
2. You are buying a flight ticket to Nairobi. In a call, ask the travel agent to get a return ticket for two.
3. You are unable to do a particular Swahili activity/exercise. As your teacher for help.

4. You are at a meeting and you realize you need to write some notes. You did not bring a notebook and pen. Ask someone to help you with these items.
5. Your friend is going to the store but you need to stay behind to complete an assignment. Ask him/her if she could buy you bread, sugar and fruits.
6. You are at the market and you would like the seller to reduce the prices of the shoes you want to buy. Ask him/her to reduce the price to the amount you want to spend.

## Kusoma

### Kununua vyakula

*Hapa ni taarifa fupi kuhusu kibanda cha Mama Siti. Soma kwa makini kisha ujibu maswali yanayofuata.*

Kila siku ya Jumamosi, mimi huenda sokoni kwani Jumamosi ni siku ya soko mjini kwetu. Kwa kawaida, mimi hununua **bidhaa** ninazohitaji kutoka kwa Mama Siti. Mama Siti ana **kibanda** kidogo katika **soko wazi** la Gikomba.

Mama Siti huuza bidhaa za aina mbalimbali. Upande mmoja, ana matunda na mboga za aina nyingi. Upande mwingine, ameweka mavazi ya mitindo mbalimbali na rangi tofauti tofauti. Kibanda chake ni safi kuliko vibanda vingine vyote hapo Gikomba.

Jana, nilihitaji kununua matunda na mboga. Kama ilivyo kawaida, nilienda kibandani kwa Mama Siti. Yeye huuza matunda na mboga kwa **bei nafuu**. Unaweza kupata vitu hivi katika **supamaketi** lakini bei yake ni ghali. Pia, katika kibanda, unaweza **kupiga bei** lakini huwezi kupiga bei katika supamaketi. Hapa kibandani kwa Mama Siti, bei za bidhaa ni bora kuliko mahali pengine popote. Kwa sababu hiyo, **wateja** wengi wanapenda kununua mahitaji yao kutoka vibandani.



*Soko wazi la Gikomba*

Jana, nilihitaji kununua matunda na mboga. Kama ilivyo kawaida, nilienda kibandani kwa Mama Siti. Yeye huuza matunda na mboga kwa **bei nafuu**. Unaweza kupata vitu hivi katika **supamaketi** lakini bei yake ni ghali. Pia, katika kibanda, unaweza **kupiga bei** lakini huwezi kupiga bei katika supamaketi. Hapa kibandani kwa Mama Siti, bei za bidhaa ni bora kuliko mahali pengine popote. Kwa sababu hiyo, **wateja** wengi wanapenda kununua mahitaji yao kutoka vibandani.

Mimi  nimekuwa mteja wa Mama Siti kwa muda mrefu. Ninapoenda kununua mboga na matunda, **yeye hunipunguzia** bei. Mara nyingine, **huniongezea** vitunguu, karoti au nyanya. Anajua asipofanya hivyo, nitanunua bidhaa kutoka kibanda kingine nikienda sokoni wakati mwingine.

Pia, ninapenda kununua kutoka kwa Mama Siti kwa sababu huuza mboga na matunda freshi. Nilipoenda sokoni jana nilikuwa ninataka kununua vitunguu, sukuma wiki, karoti, maembe, matofaa na mananasi. Nilichagua **vivurushi** sita vya sukuma wiki, **kifungu**

kimoja cha vitunguu na **vivungu** vitatu vya karoti. Pia, **nilichagua** mananasi mawili makubwa, maembe kumi na matofaa matano. Nilikuwa ninataka tikiti maji pia lakini zilikuwa bei ghali kwa hivyo sikuzikunua.

Bei ya mboga na matunda ilikuwa shilingi elfu moja mia sita hamsini na tano. Kama kawaida, nilimwomba Mama Siti **anipunguzie bei** kwa shilingi mia moja ishirini. Mama Siti hakutaka kupunguza bei. Alisema kuwa bei ya bidhaa ilikuwa imepanda sana na kuwa hangepata **faida** yoyote. Baada ya **kupiga bei** kwa muda, alikubali kunipunguzia bei kwa shilingi sitini. Pia, aliniongezea kifurushi kimoja cha sukuma, kitunguu kimoja na embe moja. Nilimshukuru na nikarudi nyumbani.

**Maswali**

Chagua jibu kutoka kwa orodha hii na ukamilishe sentensi zinazofuata.

| | | |
|---|---|---|
| kibandani | mavazi | faida |
| soko wazi | wachuuzi | mtumba |

## Zoezi

1. Soko la Gikomba ni mfano wa ……………..………………..
2. Bei bidhaa ni ghali katika supamaketi kuliko ……………..………………..
3. Mama Siti huuza mboga, matunda na ……………..………………..
4. ……………..……………….. ni watu wanaozunguka wakiuza vitu.
5. Mwuzaji anapouza bidhaa hupata ……………..………………..
6. ……………..……………….. ni mavazi ambayo yametumiwa awali na huuzwa katika soko wazi.

## Zoezi

kweli au si kweli

| | kweli | sii kweli |
|---|---|---|
| Wateja wengi wanapenda kununua mahitaji yao katika kibanda. | | |
| Mteja wa Mama Siti alinunua tikiti maji. | | |
| Mteja alinunua kifungu kimoja cha vitunguu na nanasi moja. | | |
| Bei ya matunda na mboga ilikuwa shilingi 1,655 kwa jumla. | | |

## Mazungumzo

### Kununua mavazi

Rashid ananunua mavazi katika soko wazi la Gikomba. Hapa, anazungumza na Yasmin ambaye huuza nguo za mtumba katika soko hili. Soma mazungumzo haya. Kisha, katika majozi, mtatayarisha mazungumzo kama haya. Mmoja wenu atakuwa mnunuzi na mwengine mwuzaji. Mtawasilisha mazungumzo yenu darasani.

**Yasmin:** Karibu Rashid. Habari gani?

**Rashid:** Salama tu. Na wewe je?

**Yasmin**: Salama rafiki yangu. Unataka kununua nini leo?

**Rashid**: Ninahitaji shati zuri. Saizi 14 hivi.

**Yasmin:** Nina mashati mazuri kwa bei nafuu. Nina hili la bluu, lina madoadoa meusi na kola nyeupe. Saizi ni 14 ½.

**Rashid:** Ni zuri lakini sipendi madoadoa. Pia lina vifungo vikubwa sana.

**Yasmin:** Mashati ni mengi rafiki yangu.

**Rashid:** Hebu nione shati hilo jeupe lenye mistari miembamba ya rangi ya waridi.

**Yasmin:** Bila shaka. Ni shati zuri. Kitambaa chake ni cha pamba. Lakini ni saizi 15. Litakufaa?

**Rashid:** Ninafikiri litanifaa. Bei gani?

**Yasmin:** Shilingi elfu moja mia sita.

**Rashid:** Elfu moja mia sita?! Hiyo ni bei ghali sana.

**Yasmin:** Ni ghali kidogo kwa sababu ni shati zuri sana.

**Rashid:** Ni bei ghali sana. Hutaki watoto wangu wapate chakula jameni! Nitanunua kwa shilingi elfu moja mia mbili.

**Yasmin:** Hiyo ni pesa kidogo sana. Bei ya mitumba imepanda sana. Ongeza mia mbili tafadhali.

**Rashid:** Sina pesa zingine dada.

Yasmin: Ningependa kupunguza bei zaidi lakini nitapata hasara kakangu.

**Rashid:** Hamna shida. Basi nitaenda kununua mahali pengine.

**Yasmin:** Wacha haraka kaka. Rudi tafadhali.

**Rashid:** Afadhali unipunguzie bei. Sina pesa kiasi hicho.

**Yasmin:** Sawa kaka. Kwa sababu wewe ni mteja wangu mwaminifu, nitaakuzia kwa shilingi elfu moja mia mbili.

**Rashid:** Hizi hapa pesa. Sawa. Ninashukuru.

**Yasmin:** Asante. Karibu tena kaka.

## Kusikiliza

**Katika duka la rejareja**

Duka la rejareja ni aina ya maduka ambayo huuza huuza bidhaa ambazo binadamu wanahitaji kwa matumizi ya kila siku kama vyakula, sabuni, dawa ya meno, soda, hata dawa za maumivu kama panadol. Bidhaa hizi ni bidhaa zenye faida ndogo lakini hutoka haraka haraka. Maduka ya rejareja yako kila mahali mitaani na vijijini. Hivi ni kusema kwamba, mteja anapohitaji chochote kwa haraka, hahitaji kutembea mbali kununua mahitaji yake.

Sikiliza mazungumzo baina ya Baraka na mwenye duka. Unaposikiliza, jaza jedwali hapa chini na taarifa inayohitajika. Baadaye, utajadiliana na wenzako kuhusu mambo muhimu katika mazungumzo hayo. Pata mazungumzo hapa: https://mediaspace.illinois.edu/media/t/1_1fzood54

Baraka alihitaji vitu mbalimbali. Andika ni vitu ambavyo Baraka alinunua, kiasi na bei yake katika jedwali hili

| **Bidhaa** | **Kiasi** | **Bei** |
|---|---|---|
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| 4. | | |

2. Jibu maswali haya:

(i) Bidhaa ambazo Baraka alinunua zilikuwa bei gani kwa jumla?

(ii) Baraka alimpa mwuzaji pesa ngapi?

(iii) Mwenye duka alimrudishia Baraka chenji ya pesa ngapi?






(iv) Kwa nini Baraka hataki kununua vitu zaidi?




# CHUONI

## Msamiati

Andika namba ya picha ya somo kwa kila somo katika jedwali hili.

| | | |
|---|---|---|
| Uigizaji | Fizikia | Uandishi Habari |
| Muziki | Bayolojia | Fasihi |
| Historia | Kemia | Sanaa |
| Masomo ya Kompyuta | uhasibu | Takwimu |
| Uchumi | Jiografia | Hisabati |
| Uhandisi | Mawasiliano | Udaktari |
| | Biashara | Isimu ya lugha |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1.   | 2.  | 3.  | 4.   |
| 5.   | 6.  | 7.  | 8.  |
| 9. | 10. | 11. | 12. |

|  |  |  |  |
|---|---|---|---|
| 13. | 14. | 15.  | 16. |
| 17.  | 18. | 19. | 20.  |

## Sarufi na matumizi ya lugha

**Emphatic Copula *ndi-***

Uses ***ndi***+a corresponding suffix. The suffix is the same as the one used in referential demonstratives except for noun class 1 that takes ***-ye*** instead of ***-yo***

Haya ***ndiyo*** matunda niliyonunua.

Huyu ***ndiye*** dada yangu.

These are the fruits that I bought.

1. Can be used with any demonstrative (proximate, non-proximate or referential without changing its form)

Kwa mfano:

· Huyu **ndiye** mwalimu wetu.

· Huyo **ndiye** mwalimu wetu.

· Yule **ndiye** mwalimu wetu.

| Class | Class | suffix | Mfano |
|---|---|---|---|
| 1 | M | -ye | Huyu ndi**ye** mtoto wake. |
| 2 | WA | -o | Hawa ndi**o** watoto wake. |
| 3 | M | -o | Huu ndi**o** mto wa Mississippi |
| 4 | MI | -yo | Hii ndi**yo** miti iliyokatwa. |
| 5 | JI | -lo | Hili ndi**lo** jino nililotoa. |
| 6 | MA | -yo | Haya ndi**yo** meno niliyotoa. |
| 7 | KI | -cho | Hiki ndi**cho** kiti nitakachokalia. |
| 8 | VI | -vyo | Hivi ndi**vyo** viti tutakachokalia |
| 9 | N | -yo | Hii ndi**yo** nyumba tuliyojenga |
| 10 | N | -zo | Hizi ndi**zo** nyumba tulizonjenga. |
| 11 | U | -o | Huu ndi**o** upanga alionunua. |
| 11 | U | -zo | Hizi ndi**zo** panga alizonunua. |
| 14 | U | -o | Huu ndi**o** uzembe ambao sitaki. *(uzembe-laziness)* |
| 15 | KU | -ko | Huku ndi**o** kuchoka ambao sipendi. |
| 16 | Mahali | -po | Hapa ndi**po** mahali ninapopenda. |
| 17 | Mahali | -ko | Huku ndi**ko** mahali tulikohamia. |
| 18 | Mahali | -mo | Humu ndi**mo** mahali nilimoweka vitabu vyangu. |

## Zoezi

1. Hiki …………………….. kitabu nilichosoma.
2. Hawa …………………….. wanafunzi wangu.
3. Hizi ……………………..siasa ambazo sipendi.
4. Haya …………………….. matofaa niliyopewa na nyanya.
5. Huyu …………………….. mbunge wetu. (mbunge-member of parliament).
6. Hawa …………………….. viongozi wa Afrika msahariki.
7. Hivi …………………….. vikombe ulivyoosha.
8. Hapa …………………….. nilipozaliwa.
9. Hilo …………………….. gari lake la Kiswahili.
10. Huo …………………….. ushirikiano wa Afrika ya mashariki.
11. Humu mfukoni …………………….. nilimoweka barua zako.
12. Hivi …………………….. vyama tawala Afrika ya mashariki: JAP, CCM na MRA.
13. Hapa …………………….. mahali tutakapopigia kura.
14. Huu …………………….. ukutua tuliopaka rangi.
15. Hii …………………….. mikufu aliyopewa na mpenzi wake.
16. Haya …………………….. magazeti tunayopenda kusoma.

## Kusoma

## Kusoma

### Michezo chuoni

Soma fungu hili kisha ujibu maswali yanayofuata.

Michezo yana nafasi muhimu katika maisha ya wanafunzi wa vyuo vikuu Afrika ya Mashariki. Vyuo vingi vina idara ya michezo inayotoa elimu katika michezo na tafrija. Kando na hayo, wanafunzi hujiunga na vilabu mbalimbali vya michezo katika vyuo

hivyo. Michezo hii iko katika vitengo viwili: michezo ya ndani na michezo ya nje. Mifano ya michezo ya ndani ni kama vile chesi, tenisi ya mezani, mpira wa vinyoya, karata, bao na mafumbo ya maneno. Michezo ya nje ni kama vile mpira wa kikapu, mchezo wa magongo, tenisi, riadha, uogeleaji, raga, kandanda nk. Hii michezo huchezewa katika viwanja vya michezo.

Kuna michezo inayochezwa na mtu binafsi kama vile sarakasi au mbio lakini michezo mingi huchezwa katika timu za watu wawili au zaidi. Kwa kawaida, timu kubwa kama za kandanda, raga, mpira wa kikapu huwa na kocha ambaye huwafunza wachezaji mbinu za kuucheza mchezo huo. Timu huhusika katika mashindano na timu ambayo inashinda hupata tuzo.

Kila mchezo hutumia vifaa. Hata ingawa michezo kama kandanda, mpira wa kikapu, futboli, raga na mingineyo hutumia mipira inatofautiana kwa ukubwa na maumbo. Wachezaji wa tenisi hutumia mpira mdogo wa rangi ya kijani na raketi. Wachezaji wa mchezo wa magongo na besiboli hutumia mpira mdogo na magongo. Wachezaji wa futboli huvaa helmeti kichwani. Wanariadha wa mbio za kupokezana hutumia vijiti.

Michezo ina umuhimu gani katika maisha ya mwanafunzi na vijana kwa jumla? Kwanza, ni njia ya kudumisha afya bora ya mwili na akili. Pia, ni njia ya kujenga mahusiano na wachezaji wengine. Mashindano husaidia kujenga tabia na sifa za mchezaji kama ushirikiano mwema na wengine, ustahimilivu, uaminifu nk. Zaidi ya hayo, michezo hujenga hali ya kujiamini na kujithamini. Watu wengine husema kuwa wanafunzi ambao wanajishughulisha na masomo hufaulu katika masomo yao kuliko wengine.

## Zoezi

Jibu maswali haya:

1. Besiboli hutumia vifaa gani?
2. Ni mchezo gani hutumia vijiti?

3. Toa mifano miwili ya michezo ya ndani.
4. Jukumu la kocha ni gani?
5. Timu inayoshinda katika mashindano hupata nini?
6. Taja faida mbili za kujiunga na michezo.

## Mazungumzo

**Masomo katika chuo kikuu**

| | | | |
|---|---|---|---|
| mshauri | *advisor* | kujiunga | *to join* |
| wahadhiri | *lecturers* | shule ya chekechea | *kindergarten* |
| mitihani ya kitaifa | *national exams* | idara | *department* |
| michezo ya kuigiza | *drama* | kuhitimu | *graduate* |
| sanaa na sayansi | *Arts and Sciences* | kozi | *course* |
| falsafa | *philosophy* | msingi | *foundation* |
| *Mshauri* | *advisor* | mtaala | *curriculum* |
| mafunzo | *instruction* | | |

**Amina ajiunga na Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam**

*Amina <u>anajiunga</u> na Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam. Hapa anazungumza na <u>mshauri</u> wake, Profesa Matano*

**Prof. Matano:** Hujambo? Wewe ni Amina Mlachake?

**Amina:** Sijambo Profesa Matano. Ndiyo. Mimi ni Amina. Shikamoo.

**Prof. Matano:** Marahaba. Karibu. Karibu ukae.

**Amina:** Asante sana Profesa.

**Prof. Matano:** Kama unavyojua, nitakuwa ***mshauri*** wako hapa chuoni. Nielezee kwa ufupi maisha yako ya ***awali*** kabla ya ***kujiunga*** na chuo kikuu cha Dar-es-Salaam.

**Amina:** Nilijiunga na ***shule ya msingi*** ya Samba ambapo nilisoma kwa miaka sita. Baada ya kupita ***mitihani ya kimataifa***, nilijiunga na ***shule ya upili*** ya St. Stephen, umbali wa kilomita mia moja na ishirini kutoka kijiji chetu cha Samba.

**Prof. Matano:** Kwa hivyo ulikaa katika bweni shuleni?

**Amina:** Ndiyo. Nilikaa katika bweni.

**Prof. Matano:** Ulipenda masomo gani zaidi?

**Amina:** Nilipenda kusoma Jiografia, Historia na masomo ya Dini. Pia, nilipenda ***kuigiza.*** Sikupenda kusoma ***lugha za kigeni.***

**Prof. Matano:** Vizuri. Unaweza kuendelea na masomo unayopenda katika chuo cha ***Sanaa na Sayansi***. Unajiunga na idara ya **Mtaala wa masomo na Mafunzo.** Tuna **wahadhiri** wengi wazuri na kozi mbalimbali. Ungependa kufanya nini baada ya **kuhitimu**?

**Amina:** Ningependa kuwa mwalimu wa shule ya upili baada ya **kuhitimu**.

**Prof. Matano:** Katika mwaka wa kwanza utasoma ***kozi*** kama Historia na ***Falsafa ya Elimu***, Saikolojia ya Elimu, ***Msingi*** wa Elimu na kadhalika. Pia utachagua kozi mbili ambazo ungependa kufundisha.

**Amina:** Labda nitachukua Jiografia na Masomo ya Dini.

**Prof. Matano:** Hilo ni wazo zuri. Kwa kawaida, programu yako itachukua miaka mitatu.

**Amina:** Asante sana Profesa Matano kwa ***ushauri*** wako.

## Zoezi

Kamilisha wasifu huu wa Amina na habari zinazofaa.

<u>**Wasifu wa Amina**</u>

**Jina kamili:** ………………………………………………………………………...

Mzaliwa wa: ………………………………………………………………………...

**Masomo**

Shule ya msingi: ……………………………………………………………………...

Shule ya upili: ……………………………………………………………………...

Kozi katika shule ya upili: ……………………………………………………………....

Chuo Kikuu: ……………………………………………………………………...

Chuo chake: ……………………………………………………………………...

Idara: ……………………………………………………………………...

Kozi katika chuo kikuu: ……………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………...

Jina la mshauri wake: ……………………………………………………………………..

## Writing

You have been invited to apply to a study abroad program and the director of the program has sent this form for you to fill out. Fill out the required details.

**Wasifu wako**

**Masomo**

Jina: ……………………………………………………………………...

Shule ya upili: ……………………………………………………………………

Kozi katika shule ya upili:

1. ……………………………………………………………………………..
2. ……………………………………………………………………………..
3. ……………………………………………………………………………..
4. ……………………………………………………………………………..

Chuo Kikuu: …………………………………………………………………………

Kipindi: ……………………………………………………………………………

Mwaka wa kuhitimu: ………………………………………………………………..

Chuo chako: ………………………………………………………………………...

Idara: ………………………………………………………………………………...

Kozi katika chuo kikuu:

1. ……………………………………………………………………………………..
2. ……………………………………………………………………………………..
3. ……………………………………………………………………………………..
4. ……………………………………………………………………………………..
5. ……………………………………………………………………………………..

Jina la mshauri wako: ……………………………………………………………...

# AFYA

## Msamiati

*Jifunze masamiati huu hapa {link to memrise]*

| | | |
|---|---|---|
| maumivu: pain | homa-fever | malaria-malaria |
| pumu-athsma | -umwa-be in pain | -pona-be well |
| kansa-cancer | mafua-cold | ukimwi-AIDS |
| kipindupindu-cholera | kikohozi-cough (N) | -kohoa (verb) |
| kizunguzungu-dizziness | -ugua-fall ill | ambukizo-infection, |
| -ambikiza (infect) | matibabu-treatment | -tibu (treat) |
| utapiamlo-malnutrition | -tapika-vomit | virusi-virus |
| hospitali-hospital | daktari-doctor | muuguzi-nurse |
| maabara-laboratory | dawa-medicine | -laza-admit |
| pendekeza-prescribe | -piga sindano-inject | tembe-drug |
| duka la dawa-pharmacy | -lazwa-be admitted | -vunjika-break |
| *-laza hospitali-admit in hospital* | *mfupa/mifupa-bone/bones* | |

## Sarufi na matumizi ya lugha

**Viunganishi (Conjunctions)**

Soma sentensi hizi kutoka kwa mazungumzo uliyosoma:

1. Ninapokula kitu **basi** mara nyengine ninatapika.
2. **Pia** nikikojoa nahisi mkojo unauma **pia**.
3. Usisahau kutumia chandarua **ili** mbu wasikupate.
4. Inaonekana kinga yako haikusaidia **au** imepungua nguvu.
5. **Baada ya** kumaliza hizi dawa, unaweza kula tena dawa za kinga.

**Conjunctions "vivumishi"** help connect two separate ideas in a sentence. Each of the sentences above contains two ideas which are connected by the bolded conjuctions. For isntance, the first sentence has the idea of "eating" and "vomiting." Since there is a connection between the two ideas, they are expressed in as single sentence that shows the connection. "**basi**" is used to show that connection- "When I eat, **then** sometimes I vomit." It appears that "vomiting" happens after "eating."

**Refer to the Handout for more examples of conjunctions.**

**Zoezi la darasani**
Tumia viunganishi hivi kukamilisha sentensi zinazofuata:

***kisha, kwa ajili ya, wala, kwa kuwa, badala ya, ila, tena, kwa hivyo, ingawa, ili, lakini, kwamba***

1. Nilisoma kwa bidii …………………… nipite mtihani.
2. Walienda kuona filamu …………………… ya kwenda sokoni.
3. Nilikuwa ninataka kwenda Chicago jana …………………… sikuenda kwa sababu kulikuwa na mvua.
4. Mama alitaka kununua nguo, …………………… alienda madukani.
5. Wanafunzi wote walikuja darasani …………………… Hassan.
6. …………………… mji wetu ni mdogo sana, una mahali kwingi kwa kustarehe.
7. Tulienda Florida …………………… ya arusi ya binamu yangu.
8. Nimenunua nyumba, …………………… sitakodisha nyumba mwaka ujao.
9. Sikuenda kazini leo …………………… gari langu liliharibika.
10. Mama alisema …………………… ataninunulia gari mwaka kesho.
11. Sisomi kitabu hiki, …………………… sifanyi mtihani kesho.
12. Mwanafunzi alikuja darasani bila kitabu …………………… kalamu.

## Kusoma

Magonjwa ya moyo na mishipa ya damu yamekuwa yakiongezeka kwa kasi katika nchi za Afrika kinyume miaka ya nyuma. Kati ya sababu mojawapo ni mabadiliko katika

mitindo ya maisha na lishe. Watu wengi hawana mazoezi na wanakula vyakula vyenye nishati nyingi kuliko vyenye virutubisho kwa wingi na hili linachangia sana kuongezeka kwa kasi kwa magonjwa haya.

Labda unajiuliza ni magonjwa gani haya? Hapa tunaongelea magonjwa kama shinikizo la damu la kupanda kiharusi moyo kushindwa kufanya kazi moyo kuwa mkubwa, shambulio la moyo na mengineyo. Zikiwemo sababu nyingine, magonjwa haya kwa kiasi kikubwa huchangiwa na mitindo ya maisha na lishe.

**Njia za kuzuia magonjwa ya moyo na mishipa ya damu**

Kwa kubadilisha mtindo wako wa maisha unaweza kupunguza hatari ya kupata magonjwa ya moyo, au usiyapate kabisa. Zingatia mambo yafuatayo kujikinga na magonjwa haya:

**Acha kuvuta sigara**

Uvutaji sigara na matumizi ya tumbaku ni tabia kubwa hatarishi ya magonjwa ya moyo na magonjwa mengine kama saratani. Kama hauvuti sigara, usijaribu kuvuta. Kama unakaa au unafanya kazi na watu wanaovuta jaribu kuwashauri waache kuvuta kwani kuvuta moshi wa sigara kutoka kwa mtu anayevuta kunakuweka katika hatari ya magonjwa ya moyo na saratani kutokana na kemikali zilizo kwenye moshi huo.

**Matumizi ya wastani ya pombe**

Unywaji wa pombe wa kupindukia huongeza hatari ya magonjwa ikiwemo ya moyo na mishipa ya damu. Unashauriwa kupunguza matumizi ya pombe, angalu uniti 3 -4 kwa wanaume na uniti 2 – 3 kwawanawake kwa siku. Hii inamaanisha glasi 1 ya mvinyo (wine), chupa 2 za bia za kawaida, pinti moja ya pombe kali kwa siku.

Matumizi ya wastani ya mvinyo mwekundu (red wine) katika mlo inaonekana ina faida kiafya kwa kupunguza hatari za magonjwa ya moyo.

**Mlo wenye afya**

Afya yako inajengwa na chakula unachokula. Waingereza wanasema ‘garbage in garbage out’, wakiamaanisha ukiingiza uchafu utatoka uchafu. Miili yetu inajengwa na chakula tunakula, hivyo kujenga afya njema na kujikinga na magonjwa ya moyo ni muhimu kuhakikisha unapata mlo bora.

**Zingatia yafuatayo katika mlo wako:**

**Fanya sehemu kubwa ya mlo wako kuwa matunda na mboga za majani**

Punguza matumizi ya nyama nyekundu na vyakula vya kusindikwa. Tumia samaki au kuku kama chanzo cha protini kutoka kwa wanyama.

**Punguza chumvi katika chakula chako**

Kiasi kikubwa cha chumvi kwenye mlo wako huchangia kutokea kwa shinikizo la damu la kupanda na hatimaye magonjwa ya moyo. Njia zifuatazo zitakusaidia kupunguza kiasi cha chumvi kwenye mlo wako:

Punguza kiasi cha chumvi unachoweka kwenye chakula ukiwa unapika. Weka chumvi kiasi kidogo iwezekanavyo.Usiongeze chumvi kwenye chakula kilichopikwa.Punguza ulaji wa vyakula vya kusindikwa kwani huwa vina chumvi nyingi.

**Pata vyakula vyenye madini ya potasiamu kwa wingi**

Vyakula vyenye madini ya potasiamu kwa wingi husaidia kupunguza shinikizo la damu mwilini. Vyakula kama maharagwe, njugu, spinachi, kabichi, ndizi, mapapai na tende.

**Dhibiti uzito wa mwili wako**

Uzito mkubwa wa mwili unaongeza hatari ya kutokea magonjwa ya moyo. Uzito wa katikati ya mwili (central obesity) kama kitambi ni hatarishi kwa afya yako. Kujua kama

uzito wa mwili unaendana na umbo lako, pima urefu(katika mita) na uzito katika kilo kisha gawa uzito kwa namba mraba ya urefu wako (uzito/(urefu × urefu)). BMI ya kawaida ni kati ya 18.5 mpaka 24.9

**Fanya mazoezi**

Mazoezi ya mwili kila siku ni moja ya misingi mikuu ya afya yako. Mazoezi huimarisha misuli ya moyo, kupunguza mafuta mwilini, kupunguza stresi, kudhibiti uzito wa mwili na hivyo kupunguza hatari ya magonjwa ya moyo na mishipa ya damu.

Mazoezi mbalimbali kama kukimbia, kuogelea, kuendesha baiskeli, kuruka kamba na kutembea haraka ni kati ya mazoezi unayoweza kufanya angalau kwa dakika 30 kila siku. Unaweza kujiunga na vituo vya mazoezi (gym) au kikundi cha mazoezi mtaani kwenu ili ikusaidie kushiriki kila siku.

**Pima shinikizo la damu mara kwa mara**

Shinikizo la damu la kupanda huongeza hatari ya kupata magonjwa ya moyo na mara nyingi shinikizo la damu hupanda bila kuleta dalili zozote kwa miaka mingi. Hivyo vizuri kuchukua nafasi ya kupima presha mara kwa mara, angalau mara mbili kwa mwaka.

**Fahamu kiasi cha lehemu (cholesterol) kwenye damu**

Kuongezeka kwa lehemu kwenye damu huongeza hatari ya presha na magonjwa ya moyo. Pima angalau kila baada ya miaka 5 kiasi cha lehemu kwenye damu yako. Kama kikiwa juu zaidi ya kawaida jitahidi kufanya mabadiliko ili ipungue.

**Dhibiti msongo wa mawazo na hasira**

Msongo wa mawazo na hasira huchangia kutokea kwa magonjwa ya moyo. Tengeneza njia nzuri za kukabiliana na changamoto za maisha za kila siku na kudhibiti hasira. Kuwa na marafiki karibu ambao utashirikiana nao unapokuwa na matatizo. Pia zingatia kuwa muumini mzuri wa dini yako..

https://www.jamiiforums.com/threads/njia-za-kujikinga-na-magonjwa-ya-moyo.1301476/

1. Andika njia 5 ya kujikinga na magonjwa yoyote.
2. Je, wewe hujikinga na magonjwa vipi?
3. Familia yako hujikinga na magonjwa vipi?
4. Kuna miradi ya kudhibiti magonjwa chuoni kwako? Taja hii miradi.
5. Je, kuna miradi ya kudhibiti magonjwa katika jimbo la Illinois? Taja hii miradi.

## Mazungumzo

**Maria:** Hujambo Asha!

**Asha:** Sijambo! Je, mbona hukuja shuleni jana?

**Maria:** Nilikuwa mgonjwa. Nina maumivu ya kichwa na misuli.

**Asha:** Pengine una malaria. Maumivu ya kichwa na misuli ni dalili ya ugonjwa wa malaria.

**Maria:** Mama yangu anaugua malaria pia, yeye aliienda kwa daktari juzi. Daktari alimpiga sindano na alimpa dawa ya uchungu ya Tylenol. Yeye humeza tembe mbili mara mbili kila siku baada ya kula.

**Asha:** Je, unataka kwenda kwa daktari? Mimi ninaweza kukupeleka hospitalini.

**Maria:** Ndio Asha ninataka kwenda kumwona daktari sasa hivi.

**Asha:** Basi nitakupeleka kwa daktari.

(*Wanaenda kwa daktari*)

**Nesi:** Hamjambo! Karibuni viti. Je, ninaweza kuwasaidiaje?

**Maria na Asha:** Hatujambo.

**Maria:** Mimi ninafikiri nina malaria, kwa hivyo ninataka kumwona daktari.

**Nesi:** Pole, huu ni msimu wa mvua watu wengi wana maradhi tofautitofauti hususan malaria.

**Maria:** Nimeshapoa. Je, daktari yumo ofisini?

**Nesi:** Ndio, nitakupima kwanza halafu utamwona. (*Nesi anaweka kipimajoto kwapani mwa Maria kisha anaandika joto la mwili wa Maria. Pia anamuuliza maswali na kuandika majibu chini*.)

**Daktari:** Je, kuna mgonjwa mwingine?

Nesi: Ndio. Maria njoo! (*Maria anaingia ofisini mwa daktari*)

**Daktari:** Karibu kiti. Habari za mchana?

**Maria:** Nzuri lakini ninaumwa sana na ninatapika pia.

**Daktari:** Pole sana. Usijali nitakutibu sasa hivi. (*Daktari anamkaribia na kufanya uchunguzi*).

**Daktari:** Maria nitakupiga sindano moja na nitakupa tembe za malaria. Wewe utameza tembe mbili mara mbili kila siku baada ya kula

**Maria:** Asante! (*Maria anaingia katika chumba cha ndani kupigwa sindano*).

**Daktari:** Tafadhali jaribu kutumia neti ya mbu wakati wa kulala ili kujikinga na ugonjwa wa malaria.

**Maria:** Ndiyo daktari.

**Daktari:** Haya kwaheri. Ninafikiri utapata nafuu hivi karibuni.

**Maswali**

1. Nani hakuja shuleni na kwa nini?
2. Nini ni dalili ya ugonjwa wa malaria?
3. Je, mama ya nani ni mgonjwa?
4. Mama humeza dawa mara ngapi?
5. Katika somo hili, nesi anafanya nini?
6. Katika somo hili, daktari anafanya nini?
7. Daktari anataka Maria afanye nini ili kujikinga na ugonjwa wa malaria?
8. Mdudu gani huambukiza malaria?
9. Mbu huambukiza ugonjwa gani pia?
10. Je, wewe umeshakuwa na ugonjwa wa malaria?

# Starehe na burudani

## Msamiati

*Jifunze msamiati ambao utahitaji ili kuzungumza kuhusu starehe na burudani:*
{memrise}

| | | | |
|---|---|---|---|
| burudani *(n)* | *entertainment* | starehe *(n)* | *relax* |
| kujiburudisha (v) | *entertain oneself* | tamasha *(n)* | *festival* |
| mchezo wa kuigiza | *drama* | muigizaji *(n)* | *actor* |
| tiketi *(n)* | *ticket* | waimbaji *(n)* | *singers* |
| kupiga picha *(v)* | *photography* | bendi *(n)* | *band* |
| filamu *(n)* | film/movie | ukumbi *(n)* | theater |
| klabu *(n)* | *club* | sarakasi *(n)* | *circus* |
| maonyesho *(n)* | *shows* | kucheza dansi | *dance* |
| sinema *(n)* | *movie* | shabiki *(n)* | *fan* |
| mchezo wa bao *(n)* | *board game* | karata *(n)* | *card game* |
| msanii (n) | *artist* | jina la kisanii | *stage name* |

## Sarufi

### Causative form

Refer to the notes given to you

*Patanisha vitenzi na maana. (Match the following infinitive verbs with their meanings)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | kufurahisha | a | to cause (one) to be sad |
| 2. | kuhamisha | b. | to make (one/something) play |
| 3. | kujiburudisha | c. | to make (something) compulsory |
| 4. | kuhuzunisha | d. | to cause (one) to laugh |
| 5. | kuchezesha | e. | to make (one/something) to be beautiful |
| 6. | kutendesha | f. | to make (one) happy |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 7. | kulazimisha | g. | cause to relocate/move |
| 8. | kuchekesha | h. | cause to move from one point to the other |
| 9. | kuendesha | i. | to make (one) to be entertained |
| 10. | kurembesha | j. | to make (one) do (something) |

*b. Chagua kitenzi kimoja kutoka vitenzi ulivyopewa kwenye jedwali na ujaze mapengo katika sentensi hizi.*

1. Sikupenda filamu hiyo. ………………………………………………….
2. Baba …………………………………………………. mimi na dada yangu kwenda kuona mechi.
3. Mhusika mkuu ………………………………………………….watazamaji sana.
4. Wahusika …………………………………………………. kabla ya kufanya mchezo wa kuigiza.
5. Wanafunzi walimwoba …………………………………………………. bei ya tiketi za lakini alikataa.

Change these infinitive verbs into the ***causative form.*** *Then choose 6 from the list and write sentences using the causative from.*

1. kupotea
2. kukimbia
3. kufurahi
4. kuzama
5. kusonga
6. kumeza
7. kupanda
8. kusafiri
9. kupungua
10. kuchoka
11. kuruka
12. kutembea

## Kusoma

**Vijana na burudani**

Ni jambo la kawaida siku hizi kuwauliza vijana ukiwa Tanzania au Kenya juu ya mambo ya burudani wanayoyapenda. Kitu ambacho watakisema mwanzo watakuambia ni kucheza muziki, kuangalia video na kusikiliza muziki.

Muziki katika Afrika Mashariki una historia refu. Kuna wakati katika miaka ya sabini ambapo muziki wa **bendi za asili** ulikuwa **maarufu** sana. Muziki huu ulipigwa na **wenyeji**. Kawaida, vijana walichanganyika na **watu wa makamo** kupiga na kuimba muziki huu. Muziki wa aina hii ndio uliokuwa unachezwa kwenye kumbi za starehe na hata redioni.

Katika miaka ya themanini, Afrika Mashariki **ilivamiwa** na muziki wa Zaire (sasa Demokrasia ya Jamhuri ya Kongo). **Waimbaji** kama Franco, Pepe Kale na wengineo walikuwa maarufu sana. Vijana wengi walipenda muziki wa kizaire **ijapokuwa** wengi hawakujua maana ya nyimbo za kizaire ambazo ziliimbwa kwa Kilingala (Lugha ya Zaire).

Katika miaka ya tisini **kumezuka** muziki wa **kizazi kipya** ambao ndio umepata umaarufu sana miongoni mwa vijana. Muziki huu ambao **unajulikana** kama "hip hop," nyimbo zake kawaida huimbwa kwa Kiswahili au lugha za makabila. Vijana huimba juu ya mambo tofauti ya jamii kuanzia siasa, mapenzi hadi ukimwi. Nyimbo hizi huchezwa katika kila redio ya Afrika Mashariki. Makampuni mengi ya kurekodi muziki huu katika CD na video **zimeibuka** na unaweza kununua CD au DVD yenye muziki wa kizazi kipya katika maduka ya muziki. Vijana waimbaji wameweza kujipatia **ajira** katika **fani** hii ya muziki.

Utapokuwa unatembea Afrika Mashariki usishangae kusikia nyimbo za hip-hop zikichezwa madukani, majumbani na kwenye magari. Kwa kweli vijana wa Afrika ya Mashariki wanapenda kujistarehesha kwa muziki wa kizazi kipya.

**Maswali**

1. Vijana wa Afrika ya Mashariki wanapenda kufanya nini kujiburudisha?
2. Ni muziki wa aina gani ambao ulikuwa maarufu miaka ya sabini?

3. Muziki wa miaka ya sabini ulichezwa na nani?
4. Muziki wa bendi za asili ulikuwa ukichezwa wapi?
5. Ni muziki wa aina gani ambao ulikuwa maarufu kati ya 1980-1989?
6. Taja wanamuziki wawili ambao walikuwa maarufu sana katika Afrika ya Mashariki miaka ya themanini?
7. Wanamuziki hawa wa miaka ya themanini walitumia lugha gani kuimba muziki wao?
8. Katika miaka ya tisini, ni muziki gani ambao ulikuwa maarufu Afrika Mashariki?
9. Muziki wa miaka ya sitini huibwa kwa lugha gani?
10. Nyimbo za miaka ya sitini huzungumza kuhusu nini?
11. Muziki wa kizazi kipya una umuhimu gani katika maisha ya vijana?

## Mazungumzo

Musa: Vipi Musa? Habari gani leo?

Oliech: Nzuri tu. Hamna neno. Unaenda wapi?

Musa: Ninaenda katika uwanja wa michezo wa Nyayo.

Oliech: Kuna nini?

Musa: Hujui? Kuna mechi leo.

Oliech: Mechi gani?

Musa: Kati ya timu ya Harambee Stars na Black Star kutoka Ghana.

Oliech: Ah! Mechi ni ya leo? Nilisahau bwana! Lakini mimi si shabiki wa kandanda. Sipendi michezo kwa jumla. Ndio maana nilisahau kuhusu mechi.

Musa: Kama hupendi michezo, wewe hufanya nini *kujiburudisha?*

Oliech: Kuna njia nyingi za kujiburudisha isipokuwa michezo. Mimi hupenda kuangalia sinema, kuogelea na *kujistarehesha* na rafiki zangu klabuni.

Musa: Mimi huangalia sinema mara kwa mara lakini siendi klabuni.

Oliech: Kumbe unapenda sinema? Unapenda sinema gani?

Musa: Ninapenda za filamu za Marekani.

Oliech: Kama gani?

Musa: Nyingi. Niliangalia *Fences* hivi karibuni. *Ilinihuzunisha* sana.

Oliech: *Fences*? Sijaingalia. *Haikukufurahisha?*

Musa: Sivyo. Ilikuwa nzuri lakini wahusika walikuwa na matatizo mengi.

Oliech: Mhusika mkuu ni nani?

Musa: Ni Denzel Washington. Ninapenda filamu zake zote.

Oliech: Nitaingalia nikipata nafasi.

Musa: Ni nzuri sana.

Oliech: Hebu niondoke sasa. Mchezo unaanza saa kumi. Sitaki kuchelewa.

Musa: Hamna shida. Nenda ujiburudishe tutaonana siku nyingine.

## Speaking Exercises

1. You are at a clothing store where you want to get 2-3 items. Speak with the sales person about the items that you need. Describe what you need in terms of size, color, fabric etc. Negotiate for a reasonable price.

2. You would like to take advantage of this sale and go shopping at Woolworths. You would like to go with your good friend (name) but he/she is not available. She would like you to buy some items for her. Chat with her explaining the Woolworths sale and him/her asking clarifying questions about the sale so that she can decide what you will buy for her.

3. You meet with a friend of yours on your way to a favorite activity that you like to engage in when you are free. Greet each other, tell your friend where you are going and ask him/her what he/she likes to do for entertainment. Share a little

more about what each of you likes to do, when and with whom. Also, share things that you don't like to do.

## Writing Exercises

1. The Swahili Club at your school is organizing a fundraiser for a book project to benefit Amani Children's Home in Kampala, Uganda. You will be selling food items, items of clothing and a selection of artifacts from East Africa. As the communications secretary of the club, design a flyer to go out to the community.

2. Choose a popular musician or one that you like from East Africa, research about him and write a short biography.
   a. Jina lake la kisanii ni nani ?
   b. Jina lake halisi ni nani ?
   c. Anatoka wapi ?
   d. Alizaliwa lini ?
   e. Anacheza muziki aina gani
   f. Kichwa cha wimbo wake unaoupenda zaidi ni gani ?
   g. Ameshinda tuzo zozote? Tuzo gani ?